



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

---

**HOTUBA YA WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII  
MHESHIMIWA LAZARO SAMUEL NYALANDU (MB),  
AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
YA FEDHA KWA MWAKA 2015/2016**

**Dodoma**

**Mei, 2015**

---

## **YALIYOMO**

<b>YALIYOMO .....</b>	<b>i</b>
<b>VIFUPISHO.....</b>	<b>ii</b>
<b>I. UTANGULIZI.....</b>	<b>1</b>
<b>II. MAJUKUMU YA SEKTA YA MALIASILI NA UTALII .....</b>	<b>2</b>
<b>III. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM NA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2014/2015.....</b>	<b>4</b>
A. Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2010 hadi 2015 .....	4
B. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2014/2015.....	12
<b>IV. CHANGAMOTO ZA SEKTA NA MIKAKATI YA KUZIKABILI .....</b>	<b>27</b>
<b>V. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2015/2016.....</b>	<b>28</b>
<b>VI. SHUKRANI .....</b>	<b>36</b>
<b>VII. HITIMISHO .....</b>	<b>37</b>

## VIFUPISHO

AFD	-	<i>L'Agence Française de Développement</i> (French Development Agency)
AWF	-	African Wildlife Foundation
AWHF	-	African World Heritage Fund
BTC	-	Belgian Technical Cooperation
DANIDA	-	Danish International Development Agency
FAO	-	Food and Agriculture Organization of the United Nations
FINNIDA	-	Finnish International Development Agency
FZS	-	Frankfurt Zoological Society
GEF	-	Global Environmental Facility
GIZ	-	<i>Die Deutsche Gesellschaft für Internationale Zusammenarbeit GmbH</i> (the German Society for International Cooperation)
ICCROM	-	International Centre for the Study of Preservation and Restoration of Cultural Property
ICOM	-	International Council on Museums
ICOMOS	-	International Council on Monuments and Sites
ILO	-	International Labour Organization
IUCN	-	International Union for Conservation of Nature
NCAA	-	Ngorongoro Conservation Area Authority
NGOs	-	Non Government Organizations
NORAD	-	Norwegian Development Agency
SIDA	-	Swedish International Development Agency
SNV	-	<i>Stichting Nederlandse Vrijwilligers</i> (Netherlands Development Organization)
UNDP	-	United Nations Development Program
UNESCO	-	United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization
UNODC	-	United Nations Office on Drugs and Crimes
UNWTO	-	United Nations World Tourism Organisation
USAID	-	United States Agency for International Development
WMAs	-	Wildlife Management Areas
WMF	-	World Monument Fund
WWF	-	World Wild Fund for Nature

## I. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira, Bunge lako sasa lipokee na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa Fedha 2015/2016.

2. **Mheshimiwa Spika**, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuiongoza Wizara hii yenye dhamana ya kuendeleza Utalii, kusimamia Rasilimali za Maliasili na Malikale. Aidha, natoa shukrani za dhata kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ardhi, Maliasili na Mazingira chini ya Mwenyekiti wake Mhe. James Daudi Lembeli (Mb.) ambayo ilijadili, kushauri na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016. Wizara imezingatia ushauri uliotolewa na Kamati.

3. **Mheshimiwa Spika**, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Rais, Mheshimiwa Innocent R. Sebba (Mb.) na Mheshimiwa Dkt. Grace K. Puja (Mb.). Kwa masikitiko napenda kutoa pole kwa Bunge lako Tukufu kwa kuondokewa na Hayati Kapteni John Damian Komba aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Mbinga Magharibi aliyefariki tarehe 28 Machi, 2015.

4. **Mheshimiwa Spika**, nasi Wizara ya Maliasili na Utalii katika kutekeleza majukumu yetu, tumepoteza watumishi katika maeneo mbalimbali. Baadhi yao ni: Marehemu Joseph Alphayo Rubani aliyefariki tarehe 29 Novemba, 2014 kwa ajali ya helkopta Jijini Dar es Salaam; Wahifadhi Wanyamapori wawili Marehemu Emmanuel Katambi aliyefariki kwa kung'atwa na nyoka katika Pori Tengefu la Kilombero tarehe 21 Desemba, 2014 na Marehemu George Kimaro aliyeuawa kwa kupigwa mawe na wananchi akiwa kazini katika Kijiji cha Nyamonge Wilaya ya Bukombe Mkoa wa Geita tarehe 30 Januari, 2015.

5. **Mheshimiwa Spika**, nachukua fursa hii kuwapa pole familia za marehemu kwa kuwapoteza ndugu zao. Aidha, natoa pole kwa watazania wote kutokana na ajali na majanga mbalimbali, ikiwemo kuuawa na wanyamapori. Tunamwomba Mwenyezi Mungu awape ahueni majeruhi na aziweke roho za marehemu mahali pema peponi, *Amina*.

## **II. MAJUKUMU YA SEKTA YA MALIASILI NA UTALII**

**6. Mheshimiwa Spika**, Wizara ya Maliasili na Utalii inajumuisha Sekta ndogo za Wanyamapori, Misitu, Ufugaji Nyuki, Utalii na Malikale. Jumla ya hekta milioni 28 (sawa na asilimia 33 ya eneo la Tanzania) ni maeneo yaliyohifadhiwa kisheria kama hifadhi za misitu na wanyamapori. Majukumu ya Sekta ndogo za maliasili na maendeleo ya utalii yameainishwa kama ifuatavyo:

### **i. Sekta ndogo ya Wanyamapori**

**7. Mheshimiwa Spika**, majukumu ya Sekta ndogo ya Wanyamapori ni kusimamia, kuhifadhi, kuendeleza na kuhakikisha matumizi endelevu ya rasilimali za wanyamapori kwa faida ya kizazi cha sasa na kijacho. Majukumu haya yanatekelezwa na Idara ya Wanyamapori, Shirika la Hifadhi za Taifa (Hifadhi 16), Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania. Wizara imeanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (*Tanzania Wildlife Authority – TAWA*) itakayosimamia Mapori ya Akiba 28 yenye kilometa za mraba 108,213, Mapori Tengefu 44 yenye kilometa za mraba 58,565.02 na maeneo ya wazi yaliyo nje ya Hifadhi za Taifa na Hifadhi ya Ngorongoro yenye kilometa za mraba 8,292. Aidha, Wizara inasimamia maeneo ya ardhioevu (Ramsar sites) ya Bonde la Kilombero, Malagarasi/Muyowosi, Lower Rufiji na Ziwa Natron yenye ukubwa wa kilometa za mraba 48,687.

### **ii. Sekta ndogo ya Misitu na Nyuki**

**8. Mheshimiwa Spika**, Sekta hii inachangia kiasi kikubwa cha maendeleo ya kijamii, kiuchumi, na uhifadhi wa mazingira ikiwa ni pamoja na upatikanaji wa nishati, hifadhi ya vyanzo vya maji kwa ajili ya kuzalisha umeme, umwagiliaji, uhifadhi udongo, uzalishaji wa mazao ya chakula na matumizi mengineyo. Tanzania bara ina misitu yenye ukubwa wa hekta milioni 48.1. Sekta inasimamia mashamba 18 ya miti ya kupandwa, Misitu ya Hifadhi 486 na Hifadhi za Nyuki 11. Mahitaji ya mazao ya misitu ni meta za ujazo milioni 62.3 kwa mwaka. Kiwango kinachokubalika kuvunwa ni meta za ujazo milioni 42.8 kwa mwaka. Hivyo, kuna upungufu wa meta za ujazo milioni 19.5 kwa mwaka.

### **iii. Sekta ndogo ya Utalii**

**9. Mheshimiwa Spika,** mchango wa Sekta ya Utalii katika Pato la Taifa kwa sasa ni zaidi ya asilimia 17 na inaongoza katika kuliingizia taifa fedha za kigeni ambapo imechangia takriban asilimia 25 ya fedha hizo. Sekta hii hutoa ajira kwa Watanzania, ni kichocheo cha kukua kwa uchumi katika sekta nyingine ikiwa ni pamoja na miundombinu, usafirishaji na uzalishaji wa bidhaa na huduma kwa watalii. Ukuaji wa sekta unategemea uwepo wa amani, utulivu, ubora wa huduma na miundombinu. Utalii wa Tanzania umejikita katika vivutio vya wanyamapori, upandaji milima, utamaduni, malikale, mandhari na fukwe.

#### **iv. Sekta ndogo ya Malikale**

**10. Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Sekta ndogo ya Malikale ni kulinda, kuhifadhi, kutafiti na kusimamia matumizi endelevu ya maeneo ya urithi wa utamaduni. Maeneo 129 yametangazwa kuwa kumbukumbu na urithi wa utamaduni wa Taifa, kati ya hayo 16 yanasimamiwa na Idara ya Mambo ya Kale. Maeneo yaliyobaki yako chini ya umiliki na usimamizi wa taasisi na watu binafsi. Maeneo ya Michoro ya Miambani Kolo-Kondoa, Magofu ya Kilwa Kisiwani na Magofu ya Songo Mnara ni maeneo ya Urithi wa Utamaduni wa Dunia.

### **III. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM NA MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2014/2015**

**11. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kutekeleza Majukumu yake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (2010 – 2015); Mpango Mkakati wa Wizara (2013 – 2016); Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025); Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2011/2012 - 2015/2016), Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2014/2015, Mikataba ya Kimataifa ambayo Tanzania imeridhia na Maelekezo mengine ya Kitaifa. Taarifa hizo zimeainishwa kama ifuatavyo:

#### **A. UTEKELEZAJI WA ILANI YA UCHAGUZI YA CCM YA MWAKA 2010 HADI 2015**

**12. Mheshimiwa Spika,** kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2010-2015, Wizara ilielekezwa kusimamia utekelezaji wa malengo 16 yafuatayo:

##### **i. Kuongeza msukumo katika kuendeleza ufugaji nyuki kwa ajili ya kuzalisha asali na nta kibiashara**

**13. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza msukumo wa kuendeleza ufugaji nyuki, uhamasishaji umefanyika kupitia maonesho maalum ya asali yaliyofanyika katika viwanja vya Mwalimu Nyerere Dar es Salaam Oktoba, 2012. Aidha, Wizara iliandaa na kufanikisha Kongamano la kwanza la Afrika la Ufugaji Nyuki – Apimondia lililofanyika Arusha Novemba, 2014.

**14. Mheshimiwa Spika,** ili kuendelea kuwahamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa ufugaji nyuki kwa lengo la kuwapatia kipato kwa njia ambayo ni rafiki wa mazingira, Wizara imeanzisha Siku ya Kitaifa ya Kutundika Mizinga. Siku hiyo ambayo huadhimishwa Kitaifa, Kimkoa na Kiwilaya imeanza rasmi mwaka 2013. Maadhimisho hayo yamefanyika Manyoni Mkoa wa Singida tarehe 18 Machi, 2013; Mlele Mkoa wa Katavi tarehe 18 Machi, 2014 na Handeni Mkoa wa Tanga tarehe 25 Machi, 2015. Siku hiyo, mizinga hutundikwa na baadhi hukabidhiwa kwa wananchi katika maeneo yanayofaa kwa ufugaji nyuki. Shughuli ya utundikaji mizinga huambatana na maonesho ya mazao ya nyuki na vifaa vya ufugaji nyuki.

**15. Mheshimiwa Spika,** ili kuboresha ufugaji nyuki wananchi 7,320 wa vikundi 921 vya ufugaji nyuki katika vijiji 242 kwenye

wilaya 30 walifundishwa mbinu bora za ufugaji nyuki. Mafunzo hayo yalihusu matumizi ya mizinga ya kisasa, utundikaji wa mizinga na usimamizi wa manzuki. Wizara imegawa mizinga 14,076 kwa wananchi wa mikoa 17 ya Pwani, Morogoro, Mbeya, Rukwa, Iringa, Tabora, Shinyanga, Katavi, Ruvuma, Mtwara, Lindi, Kilimanjaro, Tanga, Arusha, Singida, Manyara na Dodoma. Vilevile, Wizara imeendelea kufundisha mbinu bora za uzalishaji na ufungashaji wa mazao ya nyuki kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa katika kuzalisha na kuuza asali bora.

**ii. Kuweka utaratibu shirikishi wa upandaji miti, uvunaji na udhibiti wa moto. Ushirikishaji huo utakuwa wa sekta binafsi, NGOs na vijiji**

**16. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kushirikisha wananchi kupanda miti na kuwahamasisha kutumia mbegu bora za miti kwa ajili ya kuanzisha vitalu binafsi vya miche. Serikali ilibadilisha Siku ya Taifa ya Kupanda Miti kutoka Januari Mosi na kuwa Aprili Mosi ya kila mwaka kwa kuwa sehemu nyingi nchini kwa kipindi hicho zinakuwa na mvua za kutosha. Aidha, elimu ya kuzuia moto ilitolewa kwa umma kupitia mabango, sinema, vipeperushi, vipindi vya redio na televisheni. Kutokana na uhamasishaji huo, wananchi walishiriki kuzima moto ulioathiri hekta 1,615 katika misitu ya hifadhi ya Pugu/Kazimzumbwi, Mlima Rungwe, Chome, Magamba, Shamba la miti Shume, Kilima na Mlima Meru na Sao Hill eneo la shamba la binafsi (Green Resource).

**iii. Kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uhifadhi wa misitu na hifadhi za nyuki**

**17. Mheshimiwa Spika,** jitihada zilizochukuliwa katika kuimarisha ushiriki wa wananchi katika uhifadhi wa misitu na hifadhi za nyuki ni pamoja na kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya uhifadhi wa misitu. Wananchi 1,772 wanaoishi karibu na misitu walioneshwa picha 44 za video na kupewa machapisho 23,200 ya aina mbalimbali. Vilevile, wananchi walielimishwa kupitia matangazo ya redio vipindi 266 na televisheni vipindi 55.

**18. Mheshimiwa Spika,** eneo la misitu ambalo husimamiwa katika mipango shirikishi limefikia hekta milioni 7.7. Kati ya hizo, hekta milioni 2.4 ni misitu ya jamii na hekta milioni 5.3 ni misitu inayosimamiwa kwa ubia kati ya Serikali na wamiliki wengine. Ili kuendeleza uhifadhi shirikishi wa maeneo ya pwani, kazi ya uchoraji ramani za eneo la hekta 102.42 ilifanyika. Kazi hiyo ililenga kuainisha



maeneo ya kilimo endelevu cha mpunga kwa mkataba kwenye mikoko ya Rufiji na ufugaji kamba katika misitu ya mikoko ya Mafia.

**iv. Kuwezesha jamii zinazozunguka maeneo ya hifadhi kunufaika na rasilimali za wanyamapori na misitu**

**19. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuanzisha maeneo ya Jumuiya za Hifadhi ya Wanyamapori (Wildlife Management Areas - WMAs). Katika kipindi cha mwaka 2010 hadi 2015, Jumuiya tano zilianzishwa ambazo ni ILUMA (Kilombero na Mahenge), Ndonda (Nachingwea), Randilen (Monduli), Kidoma (Kilosa) na Mchimalu (Nanyumbu). Aidha, Jumuiya 10 zilifikia hadhi ya kuwa Jumuiya kamili (*Authorised Associations*) na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali. Jumuiya hizo ni JUKUMU (Morogoro); Magingo (Liwale); Makame (Kiteto); Makao (Meatu); Kimbanda na Kisungule Mbarang'andu (Namtumbo); Chingoli (Tunduru); Randilen (Monduli) na ILUMA (Kilombero na Mahenge).

**20. Mheshimiwa Spika,** kwa sekta ya misitu, kazi zilizofanyika kwa kushirikisha jamii ni pamoja na kubaini maeneo ya misitu; kutayarisha mipango ya usimamizi ya misitu ya vijiji na sheria ndogo; kufanya doria na tathmini ya misitu; na kufanya mapitio ya mipango ya usimamizi shirikishi wa misitu. Hekta 135,000 za misitu zimebainishwa na kuingizwa kwenye usimamizi shirikishi. Kupitia utaratibu huu, vijiji 28 vimenufaika kwa kupata vifaa vya ujenzi wa madarasa, masoko, nyumba za walimu na zahanati. Aidha, vijiji 163 vilipatiwa mafunzo ya njia mbadala ya kujipatia kipato kama vile kuotesha miche ya miti kwa ajili ya kuuza, ufugaji nyuki, ufugaji wa mbuzi, ufugaji wa samaki na kilimo cha mboga.

**v. Kuboresha miundombinu ndani ya mapori ya akiba, hifadhi za wanyamapori na misitu**

**21. Mheshimiwa Spika,** miundombinu imeimarishwa katika maeneo ya hifadhi za Wanyamapori. Kilometa 742 za barabara mpya zilitengenezwa na kilometa 1,600 za barabara na viwanja 10 vya ndege vilifanyiwa ukarabati katika Mapori ya Akiba. Wizara imejenga ofisi 12 na maghala saba ya kutunzia silaha katika Kanda za Kikosi Dhidi Ujangili na Mapori ya Akiba. Vilevile, ujenzi wa mtandao wa usambazaji maji katika Kituo cha Matambwe ndani ya Pori la Akiba Selous umekamilika.

**22. Mheshimiwa Spika,** Wizara imesafisha na kukarabati barabara ndani ya misitu zenye urefu wa kilomita 7,672 na madaraja 53 katika mashamba 18. Aidha, barabara mpya zenye urefu wa

kilomita 160.68 zimejengwa katika mashamba ya Sao Hill, Mtibwa, Wino na Rubare.

**vi. Kuendelea kuboresha mazingira ya makazi ya watumishi wanaoishi katika mazingira magumu**

**23. Mheshimiwa Spika,** Wizara imejenga nyumba 45 za watumishi kwenye Kanda za Kikosi Dhidi Ujangili na Mapori ya Akiba, nyumba tano za watumishi na ofisi mbili katika mashamba ya miti ya Mtibwa, Rubare, Rondo na Ukaguru. Aidha, Wizara imekarabati nyumba 249 kwenye mashamba ya miti, nyumba 21, nyumba mbili za kufikia wageni na ofisi 15 kwenye kanda za Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania.

**vii. Kujenga Chuo cha Utalii ili kuimarisha mafunzo ya hoteli na utalii kwa lengo la kuongeza wingi na ubora wa watumishi wa huduma hizo**

**24. Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii ulikamilisha ujenzi wa Kampasi ya Bustani, Dar es Salaam na kufunguliwa rasmi Desemba, 2011. Wakala unatoa mafunzo katika fani ya ukarimu na utalii ngazi ya Astashahada, Stashahada na mafunzo ya muda mfupi. Kutokana na kufunguliwa kwa Kampasi ya Bustani, udahili umeongezeka kutoka wakurufunzi 186 mwaka 2010/2011 hadi 218 mwaka 2014/2015.

**viii. Kukuza mwamko na kuendesha kampeni za kuwashawishi watazania kujenga utamaduni wa kutembelea vivutio vya utalii**

**25. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau, inawahamasisha watazania kutembelea vivutio vya utalii nchini. Jitihada za kukuza utalii wa ndani zilizofanyika zilijumuisha uhamasishaji na kuandaa ziara za kutembelea vivutio vya utalii nyakati za sikukuu na maonesho mbalimbali. Kampeni ya uhamasishaji inayoendesha na Bodi ya Utalii imebebwa na kauli mbiu ijulikanayo kama “**Utalii uanze kwa Mtanzania Mwenyewe**”. Mafanikio ya jitihada hizo ni kuongezeka kwa idadi ya watalii wa ndani kutoka 567,062 mwaka 2010 hadi 1,003,496 mwaka 2014.

**ix. Kupanua wigo wa aina za utalii kwa kuendeleza utalii wenye kuhusisha utamaduni, mazingira, makumbusho (historia) na michezo kama vile golfu**

**26. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendelea kupanua wigo wa Mazao ya Utalii kwa kuainisha aina nyingine za utalii kama vile utalii wa mikutano, utalii wa kiutamaduni, fukwe, ikolojia, malikale na michezo. Baadhi ya mikutano iliyotumika kuvutia watalii ni ile ya Mkutano wa Uwekezaji wa Afrika (African Investment Forum) Aprili, 2011; Mkutano wa Shirika la Utalii Duniani (UNWTO) Oktoba, 2012; African Development Bank Julai, 2012; Mkutano wa Pan Africa Oktoba, 2012; "Smart Partnership Dialogue", Juni - Julai, 2013 na Kongamano la Apimondia Novemba, 2014.

**27. Mheshimiwa Spika,** katika kutangaza utalii, Wizara ilizihamasisha timu za mpira wa miguu kutembelea vivutio vya utalii nchini. Timu ya wachezaji wa zamani wa Real Madrid ilitembelea Tanzania kuanzia tarehe 23 Agosti, 2014. Aidha, timu ya wachezaji wa zamani wa Barcelona ilitembelea nchini tarehe 10 Aprili, 2015. Utalii wa usiku umeanza kufanyika katika Hifadhi ya Taifa ya Ziwa Manyara na utalii wa kuangalia wadudu unafanyika katika Hifadhi ya Taifa Kitulo na Hifadhi Asilia ya Amani. Utalii wa makasia umeanzishwa katika Hifadhi ya Taifa Arusha – Ziwa Momela na utalii wa kutembea katika Hifadhi za Taifa Mahale na Gombe.

**28. Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha utalii ikolojia kwenye Hifadhi Asilia, jumla ya kilometa 269 za njia za watalii zilianzishwa katika Misitu ya Hifadhi Asilia ya Amani, Nilo, Chome, Uluguru, Magamba, Kilombero, Mkingu na Rungwe. Kilometa 69 za barabara kwenda kwenye vivutio vya utalii zilikarabatiwa na ujenzi wa vituo vya kupumzikia, kulala na minara (view points) ulifanyika katika hifadhi ya Chome.

**29. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilikamilisha Mwongozo wa Utalii wa Kiutamaduni mwaka 2012. Mwongozo huo unatumika kuhakiki vikundi vya utalii wa kiutamaduni vinavyofanya shughuli hizo. Hivi sasa kuna miradi 60 ya utalii wa kiutamaduni iliyopo maeneo ya Kaskazini, Pwani, Kanda ya Kati, Ziwa na Nyanda za Juu Kusini.

**30. Mheshimiwa Spika,** katika utalii wa kihistoria, Wizara ilijenga Vituo vya Kumbukumbu na Taarifa na kuweka vioneshwa katika vituo vya kumbukizi ya Dkt. David Livingstone - Ujiji Kigoma; Isimila, Iringa; na Kolo, Kondoa. Aidha, ilifanya ukarabati wa Kituo cha Caravan Serai, Bagamoyo; Tembe la Kwihara, Tabora na kuweka vioneshwa. Katika Kituo cha Magofu ya Kaole, Bagamoyo Wizara ilijenga njia za kupita wageni, mahali pa wageni kupata maelezo; kuboresha mandhari; kukarabati jengo la makumbusho ndogo ya kituo na kupanga upya vioneshwa.

**x. Kujihusisha kwa ukamilifu katika kutangaza fursa za kitalii zilizomo nchini na kuongeza bajeti ya kutangaza utalii ifanane na zile za nchi jirani**

**31. Mheshimiwa Spika,** katika kutangaza fursa za utalii zilizomo nchini, Wizara imeandaa Mkakati wa Kimataifa wa Kutangaza Utalii (2012-2016). Miongoni mwa maeneo yatakayopewa msukumo ni kuendelea kutangaza vivutio vya utalii katika masoko mbalimbali duniani ikiwa ni pamoja na masoko mapya ya nchi za Urusi, Brazil, China, India na Afrika Kusini. Hatua zilizochukuliwa katika kutangaza utalii katika masoko ya kimataifa ni pamoja na: kuandaa na kusambaza machapisho na “Country DVD” katika masoko ya utalii na balozi zetu. Wizara imefanikiwa kuweka historia ya kuviingiza vivutio vitatu vya Tanzania ambavyo ni Mlima Kilimanjaro, uhamaji wa wanyamapori katika Hifadhi ya Serengeti na Kreta ya Ngorongoro kuwa miongoni mwa Maajabu Saba Asilia Afrika “New Seven Natural Wonders of Africa”.

**32. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendelea kutangaza utalii katika vituo vya WABC-TV, CNN-America, ‘CNN headline News’ na tovuti ya CNN vya Marekani. Vilevile, iliendesha mafunzo ya utalii kwa njia ya mtandao (online destination Tanzania training) kwa wakala wa utalii nchini Marekani. Hadi mwaka 2014 wamefikia wahitimu 800 katika mpango huu. Aidha, vivutio vya utalii nchini vilitangazwa kimataifa kupitia mchezo wa mpira wa miguu kwa kuweka matangazo kwenye viwanja sita vya Ligi kuu ya mpira wa miguu ya Uingereza “English Premier League” (Agosti 2010 – Mei 2013) na katika kiwanja cha Seattle Sounders nchini Marekani (Mei 2012 – Aprili 2013).

**xi. Kufanya juhudi maalum za kutafuta masoko mapya ya utalii katika nchi zinazoinukia kiuchumi kama vile China na nchi nyingine za Asia**

**33. Mheshimiwa Spika,** ziara za kutangaza vivutio vya utalii zilifanyika katika miji ya Beijing, Shanghai na Guangzhou, nchini China. Nchini Australia, ziara za utangazaji zilifanyika katika miji ya Perth, Adelaide na Sydney. Aidha, katika kutanua wigo wa watalii wanaokuja nchini, Wizara iliandaa ziara za waandishi wa habari na mawakala wa utalii kutoka katika masoko ya Utalii ya Ufaransa, Ujerumani, Uturuki, Marekani, Australia, Ukraine, Hong Kong, Misri na Urusi kuja nchini ili kuvitangaza vivutio vya Tanzania katika nchi zao Novemba, 2013.

**xii. Kuandaa mikakati ya kuziba mianya ya uvujaji wa mapato ya utalii**

**34. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeanzisha utaratibu wa kutumia mifumo ya ki-elektroniki. Mifumo hiyo inatumika katika usimamizi wa uwindaji wa kitalii, utoaji wa vibali vya utalii wa picha na uandikishaji na utoaji wa leseni za biashara ya utalii. Kwa kutumia mifumo ya ki-elektroniki mapato kutokana na uwindaji wa kitalii, yameongezeka kutoka Dola za Kimarekani 1,867,518.99 kwa kipindi cha Julai, 2012 hadi Januari, 2013 na kufikia Dola za Kimarekani 2,320,008.78 katika kipindi cha Julai, 2013 hadi Januari, 2014 sawa na ongezeko la asilimia 24.

**xiii. Kuhimiza wawekezaji wa ndani na nje kujenga hoteli za kitalii za hadhi ya nyota 3 hadi 5**

**35. Mheshimiwa Spika,** kupitia Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), wawekezaji wameendelea kupata cheti cha motisha wanapojitokeza kujenga hoteli za kitalii zenye hadhi ya nyota 3 hadi 5. Kati ya mwaka 2010 hadi 2014, wawekezaji 222 walipewa vibali vya kuwekeza katika huduma za malazi.

**xiv. Kuzitathmini hoteli zilizopo na kuzipanga katika madaraja ya nyota zinazostahili. Wakati huo huo, kuhakikisha kuwa hoteli zinakuwa katika hali ya unadhifu**

**36. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeshiriki katika kuandaa vigezo vya kuweka huduma za malazi na migahawa katika daraja ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Aidha, imeendesha mafunzo maalum ya wataalam ya kuweka nyumba za malazi na migahawa katika madaraja ya nyota zinazostahili kwa nchi hizo. Warsha za kuhamasisha na kuelimisha wadau juu ya vigezo vitakavyotumika kupanga hoteli katika daraja zilifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na Manyara. Warsha hizo zilifuatiwa na zoezi la kupanga huduma za malazi katika daraja na kuzitunuku nyota stahiki. Katika zoezi hilo, huduma za malazi 85 zilipewa nyota ambapo Dar es Salaam zilikuwa 56, Pwani 11 na Manyara 18. Wamiliki wa huduma za malazi ambazo hazikukidhi vigezo, walishauriwa kurekebisha kasoro zilizobainishwa.

**xv. Kuendeleza jitihada za kuhifadhi mazingira katika mbuga za wanyama, misitu, fukwe za bahari na maziwa**

**37. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira imekuwa ikishiriki katika masuala mbalimbali ya uhifadhi mazingira. Masuala hayo yamehusisha ukaguzi na ushauri wa miradi ya uwekezaji katika sekta ya utalii katika maeneo ya mbuga za wanyama, misitu, fukwe za bahari na maziwa. Katika kipindi cha kuanzia Januari 2014 hadi Aprili 2015 Wizara imeshiriki katika tathmini ya mazingira kwa miradi tisa katika Mikoa ya Mwanza, Tanga, Arusha na Mara.

**xvi. Kuwavutia watalii wa nje kwa kuboresha huduma na uzalishaji wa bidhaa zenye ubora kwa kutumia teknolojia rahisi na za kisasa ili ziwavutie watalii**

**38. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha huduma na kukuza utalii, Wizara iliendesha mafunzo kwa washiriki 500 kuhusu mapishi, huduma ya vyakula na vinywaji, usafi wa nyumba na huduma kwa mteja, mapokezi ya wageni na uongozaji watalii. Mafunzo hayo yalifanyika katika Mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Pwani, Dodoma, Iringa, Njombe, Mbeya, Mwanza na Kilimanjaro. Vilevile, Wizara ilitoa mafunzo ya ujasiriamali na utalii kwa vikundi vinne katika Wilaya za Pangani na Bagamoyo. Mafunzo hayo yalihusu uongozaji watalii, kutengeneza batiki na sanaa nyingine za mikono, huduma kwa mteja, usafi na mapishi.

**xvii. Kuhakikisha kuwa kuna usafiri wa uhakika wa ndege ili kuimarisha utalii**

**39. Mheshimiwa Spika,** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa Sekta ya anga imefanikiwa kuyashawishi Mashirika ya ndege ya Qatar Airways, Fly Dubai, Air Seychelles na Turkish Airlines kuanzisha na kuongeza idadi ya safari na ukubwa wa ndege. Kufuatia hatua hii, Shirika la ndege la Fly Dubai limeanzisha safari zake nchini na mashirika ya Qatar Airways na Emirates yameongeza idadi ya safari. Aidha, Shirika la ndege la FastJet limeongeza safari za ndani na kuanzisha safari kati ya Tanzania na nchi jirani za Zambia, Zimbabwe, Afrika Kusini na Uganda.

## **B. UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2014/2015**

**40. Mheshimiwa Spika**, katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka 2014/2015 Wizara imezingatia ushauri wa kamati na ahadi zilizotolewa bungeni. Utekelezaji huo umefanyika kisekta kama ifuatavyo:

### **i. Sekta Ndogo ya Wanyamapori**

#### **a. Sheria na Kanuni**

**41. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza Sheria ya Uhifadhi Wanyamapori Na.5 ya mwaka 2009 (Sura 283), rasimu mbili za Kanuni zimetayarishwa. Rasimu hizo ni Kanuni za Usimamizi wa Mapori Tengefu na Kanuni za Usimamizi wa Shoroba, Maeneo ya Mazalia na Mtawanyiko wa Wanyamapori.

#### **b. Uhifadhi na Usimamizi wa Wanyamapori**

**42. Mheshimiwa Spika**, hatua za uhifadhi na usimamizi wa wanyamapori zilijumuisha kuendesha siku za doria 103,895 ndani na nje ya Mapori ya Akiba. Katika doria hizo watuhumiwa 1,082 walikamatwa na jumla ya kesi 988 zilifunguliwa katika mahakama mbalimbali. Kesi 424 zenye watuhumiwa 259 zilimalizika kwa wahalifu kulipa faini ya Sh. 268,250,000 na wengine 18 kufungwa jela jumla ya miezi 26. Kesi 256 zenye watuhumiwa 614 zinaendelea katika mahakama mbalimbali.

**43. Mheshimiwa Spika**, nyara za Serikali zilizokamatwa ni nyamapori yenye kilogramu 9,658.5 na meno ya tembo 182 yenye uzito wa kilogramu 256. Nyara nyingine ni kucha za simba 451; meno ya simba 65; ngozi 60 za wanyamapori mbalimbali; ndege hai 65 wa aina mbalimbali; kenge 149; lita 10 za mafuta ya simba na matenga 50 ya samaki. Mifugo na mali nyingine zilizokamatwa ni pamoja na ng'ombe 17,489; mbao 1,828; magogo 130 na magunia ya mkaa 915. Aidha, silaha 132 za aina mbalimbali zilikamatwa na kati ya hizo bunduki 84 ni za kivita.

#### **c. Ushirikishwaji Jamii katika Uhifadhi wa Wanyamapori**

**44. Mheshimiwa Spika**, Wizara imeendelea kuhamasisha uanzishaji wa Maeneo ya Jumuiya za Uhifadhi wa Wanyamapori (WMAs). Jumuiya za WAGA (Iringa Vijijini na Mufindi) na UMEMARUWA (Mbarali na Wanging'ombe) zimefikia hatua ya mwisho ya kuanzishwa. Aidha, jumuiya ya ILUMA (Kilombero na Ulanga) na

JUHIWANGUMWA (Rufiji) zimeelekezwa kufanya marekebisho ya mpango wa matumizi ya rasilimali ili ziweze kuandikishwa. Katika mwaka 2014/2015, mgao wa fedha kwa Jumuiya za Jamii za Uhifadhi wa Wanyamapori (WMA) nane zilizoandikishwa ulikuwa ni Dola za Kimarekani 180,711. Vilevile, Halmashauri za Wilaya 26 zinazopakana na Hifadhi zilipata mgao wa fedha wa asilimia 25 wa Dola za Kimarekani 314,286.62.

**d. Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA)**

**45. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania imeanzishwa kwa Tangazo la Serikali Na. 135 la Mei, 2014. Serikali imeipa Mamlaka nguvu ya kisheria ya kiutendaji kupitia Tangazo la Serikali Na. 20 la tarehe 15 Januari, 2015. Wizara ipo kwenye hatua za mwisho za kuunda Bodi ya Mamlaka ili ianze kazi yake mara moja ikiwa ni pamoja na kuajiri Mkurugenzi Mkuu na watendaji wengine.

**e. Ulinzi wa Maisha ya wananchi na Mali zao dhidi ya Wanyamapori**

**46. Mheshimiwa Spika,** Katika kushughulikia wanyamapori wakali na waharibifu kwenye wilaya zenye matatizo sugu, siku za doria 1,264 ziliendeshwa katika wilaya 25. Pamoja na juhudi hizo, Wizara ilipokea taarifa za kuuawa wananchi 42 katika Wilaya za Kilwa, Tabora, Tunduru na Ilemela. Sh. 36,300,000 zililipwa kama kifuta machozi kwa ajili ya wananchi 45 waliopoteza maisha na waliojeruhiwa katika Wilaya za Singida, Loliondo, Masasi, Serengeti, Tarime, Mpanda, Tabora, Tunduru na Ilemela.

**47. Mheshimiwa Spika,** Sh. 93,659,000 zililipwa kama kifuta jasho kwa ajili ya ekari 2,095.4 za mazao zilizoharibiwa na wanyamapori. Aidha, ng'ombe 15, mbuzi 12, punda mmoja, kondoo wanane na nguruwe wawili waliuawa na simba katika Wilaya za Nanyumbu na Babati. Kifuta jasho cha Sh. 1,400,000 kililipwa kwa wananchi ambao mifugo yao iliuawa na wanyamapori.

**f. Migogoro ya Mipaka kati ya Wananchi na Hifadhi za Wanyamapori**

**48. Mheshimiwa Spika,** jitihada za utatuzi wa migogoro katika Hifadhi za Wanyamapori zinaendelea ambapo kumekuwa na hatua za maridhiano kati ya Wizara na wadau. Katika kufikia maridhiano, Kamati za Ulinzi na Usalama za Mikoa, Halmashauri za Wilaya na



Wananchi wamehusishwa. Baadhi ya maeneo yenye migogoro ya muda mrefu iliyotatuliwa ni Hifadhi ya Taifa Mikumi, Pori la Akiba Mkungunero na Msitu wa Hifadhi Kazimzumbwi. Aidha, mgogoro kati ya Pori la Akiba Mkungunero na Hifadhi ya Jumuiya ya Jamii ya MAKAME ulisuluhishwa kwa kurejesha eneo lenye ukubwa wa kilometa za mraba 50.5 kwa wamiliki wa hifadhi hiyo ya jamii. Wizara kwa kushirikiana na wadau inaendelea kutafuta ufumbuzi wa migogoro iliyosalia.

#### **g. Mpango Mkakati wa Kuzuia Ujangili**

**49. Mheshimiwa Spika**, katika jitihada za kupambana na ujangili, Mpango Mkakati wa miaka mitano (National Anti poaching Strategy 2014 - 2019) ulizinduliwa Novemba, 2014. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) imeandaa mpango kazi wa mwaka mmoja ambao utatumia Dola za Kimarekani 10,000,000 kwa utekelezaji. Mpangokazi huo ulizinduliwa rasmi Aprili, 2015. Mashirika ya UNDP, United Nations Office on Drugs and Crime (UNODC) na Benki ya Dunia yameahidi kuchangia utekelezaji wa mkakati huu.

**50. Mheshimiwa Spika**, Wizara imejenga uwezo wa kusimamia maliasili na uendelezaji wa utalii kwa kushirikiana na wadau. Wizara kwa ufadhili wa Taasisi ya Howard Buffet imenunua magari 7 kwa ajili ya Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi na Pori la Akiba Selous. Aidha, Taasisi hiyo inashirikiana na Wizara kujenga mabweni mawili, maktaba na imenunua vifaa vya mafunzo. Pia, imenunua helikopta mbili zitakazotumika kufanya doria. Taasisi ya "Wildlife Conservation Foundation of Tanzania (WCFT) imechangia magari sita ya doria. Kwa kushirikiana na AWF, Wizara inaanzisha mradi wa kutumia mbwa kutambua nyara katika viwanja vya ndege wa JNIA, KIA na Bandari ya Dar es Salaam.

**51.** Kupitia mashirikiano na Serikali ya Watu wa Marekani, Askari Wanyamapori wamepatiwa mafunzo ya kukabiliana na ujangili pamoja na vifaa. Aidha, kupitia ushirikiano na Serikali ya Ujerumani, Wizara imeanzisha mradi wa uhifadhi Pori la Akiba Selous na Hifadhi ya Taifa Serengeti, ambapo magari 11 yamenunuliwa, ndege moja aina ya "Cessna 206" imetolewa, na kazi ya kuhesabu wanyamapori (hususan tembo) imefanyika kwa ushirikiano na TAWIRI. Kupitia ushirikiano na Kampuni ya Ortello Business Corporation (OBC), Wizara imepata magari matano kwa ajili ya doria. Kupitia ushirikiano na Kampuni ya Uranium One Wizara imepokea magari mawili ya doria.

#### **h. Mfuko wa Uhifadhi Wanyamapori Tanzania**

**52. Mheshimiwa Spika,** Mfuko ulikadiriya kukusanya Sh.16,980,000,000. Hadi Machi 2015, Sh.6,998,599,369 zilikusanywa sawa na asilimia 41.2 ya lengo. Fedha hizo zimetumika kwa kazi za uhifadhi wa Wanyamapori, utafiti na mafunzo, ukarabati wa miundombinu ndani ya Mapori ya Akiba na kugharimia uendeshaji wa Vyuo na Taasisi za wanyamapori.

#### **i. Vyuo vya Taaluma ya Wanyamapori**

**53. Mheshimiwa Spika,** Chuo cha Usimamizi na Uhifadhi wa Wanyamapori Mweka kilidahili wakurufunzi 616 hivyo kuvuka lengo la kudahili wakurufunzi 580. Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi kilidahili wakurufunzi 415 na kuvuka lengo la wakurufunzi 400. Aidha, Kituo cha Elimu kwa Jamii Likuyu Sekamaganga kilitoa mafunzo kwa wananchi 83. Kazi nyingine zilizofanyika ni ukarabati wa nyumba iliyokuwa makazi ya mtumishi na kubadilishwa kuwa bweni, ujenzi wa madarasa mawili, vyoo na bafu kwa Chuo cha Mweka. Wakufunzi watatu walihitimu mafunzo, mmoja katika Shahada ya Uzamili na wawili Shahada ya Uzamivu. Aidha, Chuo cha Pasiansi kilipokea msaada wa vifaa mbalimbali vikiwemo mahema 25 na magari saba. Vilevile, wakufunzi 16 waliwezesha kushiriki mafunzo ndani na nje ya nchi.

#### **j. Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania (TAWIRI)**

**54. Mheshimiwa Spika,** Utafiti wa aina za nyuki kwa kutumia muonekano ulifanyika na matokeo yamebaini kuwepo kwa aina tatu za nyuki wanaouma na aina saba za nyuki wasiouma. Utafiti wa mahusiano kati ya nyuki na mimea umefanyika katika Wilaya 60 na kukusanya sampuli 3,000 za chavua. Sampuli 1,500 zimefanyiwa uchunguzi na matokeo ya utafiti yatasaidia kutengeneza ramani ya kiikolojia kuonyesha kanda za asali na mimea. Taasisi ilitoa mafunzo ya njia muafaka za ufugaji nyuki kwa wafugaji 255. Mafunzo hayo yalifanyika katika Wilaya za Hanang, Kiteto na Simanjiro. Aidha, Taasisi inaendelea na ujenzi wa maabara ya utafiti wa nyuki.

**55. Mheshimiwa Spika,** Taasisi ilifanya sensa ya wanyamapori katika mifumo ikolojia ya Serengeti, Tarangire-Manyara, Katavi-Rukwa, Burigi-Biharamulo-Kimisi, Malagarasi-Moyovosi Ramsar site, Selous-Mikumi, Ruaha-Rungwa na Hifadhi za Mkomazi na Saadani. Wizara inaendelea na uchambuzi wa takwimu kabla ya kutangaza rasmi matokeo.

**56. Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Utafiti wa mbwa-mwitu umetambua makundi 20, yakiwa na mbwa wapatao 250 kwenye eneo la Loliondo, Ngorongoro na Serengeti. Makundi sita yenye mbwa 80 yamehamishiwa Hifadhi ya Taifa Serengeti kutoka maeneo ya Loliondo ambapo yalikusishwa na migogoro kwenye makazi ya binadamu. Mienendo ya mizunguko ya makundi manne inafuatiliwa kwa kutumia “Satellite GPS radio”. Matokeo ya awali yanaonesha makundi yote yanaendelea kuishi ndani ya eneo la mfumo-ikolojia wa Serengeti na yanaendelea vizuri.

**k. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)**

**57. Mheshimiwa Spika,** jumla ya Sh.1,100,000,000 zimetumika kuwezesha upatikanaji wa chakula (mahindi gunia 22,000) kwa wafugaji waishio ndani ya Hifadhi. Vilevile, Sh.103,530,000 zimetumika kununua chakula kwa ajili ya shule zote za msingi zilizopo katika eneo la Hifadhi.

**58. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ilinunua magari matano kwa ajili ya kuimarisha huduma za uhifadhi. Ukarabati wa nyumba za watumishi ulifanyika katika vituo vya Kreta na ujenzi wa uzio kuzunguka nyumba za watumishi eneo la Kamyn unaendelea. Vilevile, matengenezo ya barabara zenye urefu wa kilomita 26 kati ya Nasera Rock na Kijiji cha Piyaya umekamilika.

**1. Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)**

**59. Mheshimiwa Spika,** Shirika limelenga kutatua migogoro ya mipaka na kutunza shoroba kwa kuwezesha Hifadhi zote 16 kusaidia vijiji kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi. Hifadhi za Taifa Ruaha, Udzungwa, Saadani, Mahale, Mikumi na Mkomazi zimekamilisha mipango ya matumizi bora ya ardhi katika baadhi ya maeneo yanayozizunguka. Kazi hiyo imefanyika kwa ushirikiano na Halmashauri za Wilaya husika. Kilomita za Mraba tano za Ushoroba wa Bujingila unaounganisha Hifadhi ya Kitulo na Mlima Rungwe umefunguliwa. Vilevile, Shirika kwa kushirikiana na uongozi wa Wilaya za Monduli, Karatu, Babati na Mbulu limefanya mikutano ya uelimishaji kwa wananchi kuhusu matumizi sahihi ya shoroba na kukubaliana utaratibu wa kuzisimamia. Kazi hiyo inaendelea katika Wilaya za Siha, Longido, Simanjiro na Kiteto.

**60. Mheshimiwa Spika,** Shirika liliendelea kuimarisha miundombinu katika Hifadhi ili kuboresha mazingira ya kazi na shughuli za utalii. Shirika limejenga na kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 2,285 katika Hifadhi za Taifa za Ruaha, Serengeti, Mikumi, Katavi, Arusha, Tarangire, Manyara na Saadani. Aidha, barabara mpya yenye urefu wa kilomita 30 imejengwa katika Hifadhi ya Taifa Arusha. Kilomita 45.6 za njia za milimani zilikarabatiwa katika Hifadhi za Udzungwa na Arusha. Vilevile, katika Hifadhi ya Kilimanjaro barabara za Kilema – Horombo kilomita 19 na Londorosi – Shira kilomita 24.4 zimekarabatiwa. Uwanja wa Ndege wa Kalolwa katika Hifadhi ya Mahale umeongezwa urefu wa mita 290. Viwanja vingine vitano katika Hifadhi za Serengeti na Ruaha vyenye urefu wa kilomita 7.6 viliwekewa changarawe na kushindiliwa (Serenera kilomita 2.2; Kogatende kilomita 1.5; Lobo kilomita 1.5; Msembe kilomita 1.2 na Jongomero kilomita 1.2).

**61. Mheshimiwa Spika,** Shirika lilitokeleza miradi ya umeme jua katika Hifadhi za Mikumi, Gombe, Mahale, Ziwa Manyara, Saadani na Rubondo. Ukarabati wa nyumba nne umefanyika katika Hifadhi ya Arusha na ujenzi wa nyumba 10 za watumishi katika Hifadhi za Taifa za Tarangire (5), Ruaha (4) na Arusha (1). Huduma kwa watalii na kuboresha maliwato zilifanyika katika Mlima Kilimanjaro kwa kuanza na ujenzi wa vyoo vitatu vyenye mashimo sita kila moja katika vituo vya Karanga, Simba na Cave station. Vilevile, uboreshaji wa malango mawili ya wageni ya Mweka na Rongai umekamilika.

**ii. Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki**

**a. Sera na Sheria**

**62. Mheshimiwa Spika,** mapitio ya Sera ya Taifa ya Ufugaji Nyuki ya mwaka 1998 yanaendelea. Kazi ya kukusanya maoni ya awali kutoka kwa wadau katika Kanda za Kaskazini, Magharibi, Ziwa, Kati, Kusini, Mashariki na Nyanda za juu Kusini ilifanyika. Rasimu ya awali imekamilika na itapitiwa tena na wadau kwa ajili ya kuiboresha kabla ya kupelekwa kwenye mamlaka husika kwa ajili ya kuridhiwa.

**63. Mheshimiwa Spika,** Wizara ilifanya mikutano ya wadau katika Kanda za Mashariki, Kati, Kaskazini, Ziwa, Kusini, Magharibi na Nyanda za Juu Kusini kwa ajili ya kukusanya maoni na kutayarisha taarifa ya utekelezaji wa Programu ya Misitu na Nyuki (2001 - 2010). Taarifa hiyo itatumika kuandaa Programu mpya ya Misitu na Nyuki (2016 - 2021) baada ya kuridhiwa kwa Sera ya Taifa ya Misitu.

**b. Vyuvo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki**

**64. Mheshimiwa Spika,** wakurufunzi 375 wamedahiliwa ukilinganisha na 239 kwa mwaka 2013/2014 kama ifuatavyo: Chuo cha Misitu Olmotonyi, Arusha (266); Chuo cha Viwanda vya Misitu, Moshi (30) na Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki, Tabora (79). Kwa kuzingatia mahitaji ya wataalamu wa viwanda vya misitu nchini, mtaala kwa ajili ya kuanzisha kozi ngazi ya Stashahada umeandaliwa na Chuo cha Viwanda vya Misitu.

**65. Mheshimiwa Spika,** mazingira ya vyuvo vya misitu na nyuki yameboreshwa kwa kuongeza vifaa vya kisasa katika karakana za mafunzo ya Chuo cha Viwanda vya Misitu; kukarabati nyumba tisa za watumishi na jengo la zahanati katika Chuo cha Misitu Olmotonyi. Vilevile, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kimeandaa ramani na makadirio ya gharama kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya mkufunzi.

**c. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)**

**(i) Usimamizi wa Mashamba ya Miti**

**66. Mheshimiwa Spika,** Wakala ulipanda miche 19,419,823 kwenye maeneo mapya hekta 6,389.83 na maeneo yaliyovunwa hekta 1,495.73 katika mashamba ya miti. Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na kuondoa magugu kwenye eneo la hekta 31,598.6, kupogoa hekta 5,393.51 na kupunguza miti kwenye hekta 1,454.5. Miundombinu imeimarishwa kwa kukarabati barabara zenye urefu wa kilomita 2,391.22 na kujenga barabara mpya zenye urefu wa kilomita 175.6 ndani ya mashamba ya miti. Usafi wa barabara za kuzuia moto zenye urefu wa kilomita 2,414.21 umefanyika kwenye mashamba 10 na kazi ya kusafisha mipaka yenye urefu wa kilomita 85 imefanyika katika mashamba matano. Minara miwili ya kufuatilia matukio ya moto ilijengwa katika Mashamba ya Sao Hill na Rubya. Aidha, ulinzi wa misitu katika mashamba 18 ulifanyika kwa kuendesha doria-siku 115,825.

**67. Mheshimiwa Spika,** Wakala umeanzisha mashamba mapya ya miti Ruvu Kusini na Korogwe, yenye eneo la hekta 42,805 ili kukidhi upatikanaji endelevu wa malighafi kwa viwanda vya mbao na samani nchini. Hadi Machi, 2015 hekta 110.7 zimepandwa miti aina zifuatazo: misaji hekta 74; mikaratusi hekta 26.7; na mianzi hekta 10. Aidha, soroveya ilifanyika kwenye eneo la hekta 21,583.1 ili kugawa

viunga katika Mashamba ya Miti ya Kawetire, Mbizi, Mtibwa, Rondo na Wino-Ifinga.

**(ii) Usimamizi wa Rasilimali za Misitu na Nyuki**

**68. Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha kuwa Sheria, Taratibu na Kanuni zinazingatiwa katika uvunaji na biashara ya mazao ya misitu, doria-siku 39,309 ziliendeshwa katika maeneo mbalimbali ya misitu ya asili. Kutokana na doria hizo, mbao 43,833, magogo 1,076, mkaa magunia 50,715 na misumeno ya moto (chain saws) 64 vilikamatwa. Vilevile, matanuru 236 ya mkaa yaliyokutwa ndani ya hifadhi za misitu yaliharibiwa. Watuhumiwa 89 kesi zao zipo katika hatua mbalimbali mahakamani na wahalifu 137 walitozwa faini. Aidha, wavamizi wa misitu waliondolewa katika hifadhi 23.

**69. Mheshimiwa Spika,** kamati za kusimamia uvunaji wa mazao ya misitu katika Halmashauri 47 za wilaya, ziliwezesha kuendesha vikao vya kujadili maombi ya uvunaji. Aidha, elimu ya uelewa wa taratibu za kisheria za uvunaji na biashara ya mazao ya misitu ilitolewa kwa wafanyabiashara 1,621 katika kanda za Mashariki, Kusini, Kati, Ziwa na Kaskazini.

**70. Mheshimiwa Spika,** Wakala uliandaa mipango 10 ya usimamizi wa misitu katika Kanda za Kaskazini na Kusini na kuwezesha wilaya 15 za Kanda ya Ziwa na Mashariki kuandaa mipango ya uvunaji. Kazi ya kuimarisha mipaka imefanyika kwa kuhakiki mipaka yenye urefu wa kilomita 1,419; kusimika maboya 1,321; kuweka vibao 1,996 vya alama ya tahadhari; na kuchimba mashimo 653 ya mwelekeo. Aidha, mipaka yenye urefu wa kilomita 2,203 imesafishwa. Miche ya miti 1,785,579 ilikuzwa na kupandwa katika mipaka na maeneo ya misitu yaliyoharibiwa katika misitu 12 iliyopo katika Kanda za Mashariki, Kusini, Kati na Kaskazini.

**71. Mheshimiwa Spika,** ili kupanua wigo wa utalii ikolojia katika misitu ya hifadhi, Wakala ulianzisha kambi moja ya kupumzikia wageni na njia za kuvinjari zenye urefu wa kilomita sita katika Msitu wa Hifadhi Pugu. Jengo la ofisi na kambi mbili za kupumzikia (campsites) zilijengwa katika Msitu wa Hifadhi Vikindu na hatua za kuweka umeme zinakamilishwa. Vilevile, ukarabati wa mabanda manne ya kuhudumia watalii umefanyika katika msitu wa Kimboza na njia za kuvinjari zenye urefu wa kilomita 23 zimesafishwa katika Hifadhi ya Misitu Asilia ya Uluguru na Mkingu. Katika hifadhi za Rungwe na Kilombero, barabara zenye urefu wa kilomita 35, njia za kuvinjari zenye urefu wa kilomita 110 na kambi 18 za kupumzikia wageni zimejengwa.

### **(iii) Ushirikishwaji wa Jamii**

**72. Mheshimiwa Spika,** Kamati 36 za maliasili za vijiji katika Kanda ya Kati zilipatiwa mafunzo ya usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu. Vikundi 150 na shule mbili katika kanda za Kati, Magharibi, Ziwa na Nyanda za Juu Kusini zilipatiwa vifaa vya bustani na mbegu za miti. Hatua hiyo imewawezesha kuotesha miche ya miti 3,275,376 kwa ajili ya kupanda kwenye maeneo yao. Aidha, miche 311,630 ilitolewa kwa vijiji 23 vinavyozunguka Mashamba ya Miti ya Buhindi (20,000), Mbizi (63,100) na Sao Hill (228,530) ili kuanzisha bustani na mashamba ya miti katika maeneo yao.

**73. Mheshimiwa Spika,** vikundi 86 katika wilaya za kanda ya Kati na Kusini vilipatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki. Aidha, vijiji 154 vinavyopakana na misitu ya hifadhi na mashamba ya miti vimewezeshwa kuanzisha miradi ya ufugaji nyuki kwa kupewa mafunzo, mizinga na vifaa vya kinga. Mizinga 600 imetolewa kufanikisha miradi hiyo na mizinga mingine 380 ipo katika hatua ya mwisho ya kutengenezwa kwa ajili ya kugawiwa vikundi vilivyopatiwa mafunzo. Vituo viwili vya uzalishaji wa makundi ya nyuki vinajengwa Masasi na Vikindu ili kukidhi mahitaji ya ufugaji nyuki. Maeneo yenye hekta 3,772 yametengwa kwa ajili ya kuanzisha hifadhi za nyuki katika Kanda za Kati na Mashariki.

### **(iv) Kutoa Elimu kwa Umma**

**74. Mheshimiwa Spika,** jamii imeelimishwa kuhusu usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za misitu na nyuki kupitia vipindi 50 vya redio, 137 vya televisheni, maonesho 35 ya sinema na machapisho nakala 1,915. Elimu ilitolewa kupitia maonesho ya Sabasaba, Nanenane, siku za Kitaifa za kupanda miti na kutundika mizinga. Kampeni na mafunzo dhidi ya moto zilifanyika kwenye vijiji 668 vilivyopo kando ya misitu ya hifadhi na mashamba ya miti. Vifaa 644 vya kuzimia moto viligawiwa kwa wanavijiji wakati wa kampeni hizo.

### **(v) Kujenga Uwezo wa Watumishi na Taasisi za Misitu na Nyuki**

**75. Mheshimiwa Spika,** katika jitihada za kuimarisha usimamizi wa rasilimali za misitu na nyuki, Wakala umewezesha watumishi 104 kupata mafunzo. Kati ya hao, watumishi 44 walipatiwa

mafunzo ya muda mrefu na 60 mafunzo ya muda mfupi. Vilevile, Wakala umewezesha vyo na taasisi za Misitu na Ufugaji Nyuki kutelekeza shughuli za maendeleo. Wakala kwa kushirikiana na TAWIRI wanaendelea na ujenzi wa maabara ya utafiti wa nyuki na mazao yake. Mafunzo ya afya ya nyuki yaliendeshwa kwa wataalamu 14 wa ufugaji nyuki mwezi Novemba, 2014 katika Kituo cha Utafiti wa Wanyamapori Njiro. Wakala umekarabati nyumba 82 za watumishi kwenye mashamba ya miti na ofisi za kanda.

#### **(vi) Kongamano la Ufugaji Nyuki Apimondia 2014**

**76. Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoliarifu Bunge lako tukufu katika hotuba ya 2014/2015 kuhusu Kongamano la Apimondia, napenda kutoa taarifa kuwa Kongamano hilo limefanyika kwa mafanikio na kuhusisha washiriki 941. Kati ya hao, washiriki 839 walikuwa watanzania na 102 walikuwa wageni kutoka nchi 26. Kongamano limetoa elimu kuhusu mbinu za kulinda ubora wa mazao ya nyuki; umuhimu wa nyuki katika uchavushaji wa mimea; magonjwa ya nyuki; na jinsi wafugaji nyuki watakavyokabiliana na mabadiliko ya tabia nchi. Wafugaji nyuki walipata fursa ya kubadilishana uzoefu, kupata masoko ya mazao ya nyuki na vifaa vya ufugaji nyuki kutoka ndani na nje ya nchi. Kufuatia Kongamano hilo, Chama cha Kuendeleza Ufugaji Nyuki Tanzania kitakachowaunganisha wadau wa ufugaji nyuki kipo katika hatua za mwisho za uanzishwaji.

#### **(vii) Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF)**

**77. Mheshimiwa Spika,** Mfuko ulikadiria kukusanya **Sh.5,357,540,000** kutoka vyanzo vyake. Hadi Machi 2015, Mfuko umekusanya **Sh.3,204,020,915** sawa na asilimia 60 ya makadirio ya makusanyo kwa mwaka 2014/2015. Mfuko ulikadiria kutumia **Sh.1,992,603,700** kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa miradi 173 ya wadau wa misitu na ufugaji nyuki ikiwemo miradi mipya 97. Hadi Machi 2015, **Sh.564,263,386** zimetumika kwa ajili ya miradi midogo 114.

#### **(viii) Wakala wa Mbegu za Miti (TTSA)**

**78. Mheshimiwa Spika,** hadi Machi 2015, Wakala ulikusanya kilo 15,395 za mbegu za miti na kuuza kilo 12,907 zenye thamani ya Sh. 221,100,429. Aina za mbegu za miti zilizouzwa ni 140 na kati ya hizo, miti ya asili ni 50 ambayo ni sawa na asilimia 36 na iliyosalia ni mbegu za miti ya kigeni. Ili kuhakikisha upatikanaji endelevu wa



mbegu za miti, Wakala ulianzisha vyanzo saba za mbegu za miti za Msenefu, Mwiluti, Mpaaulonia, Mkongo, Mlonge, Mkaratusi na Mjohoro huko Lushoto Tanga, Kigwe Dodoma na Mkundi Morogoro.

**79. Mheshimiwa Spika,** miche 98,364 yenye thamani ya Sh.61,055,700 iliuzwa. Miche iliyouzwa zaidi ni Mitiki, Miembe, Michungwa, Mikangazi, Mgrevilea na Mgolimazi. Hali kadhalika, Oktoba, 2014 Wakala uliendesha mafunzo ya muda mfupi kuhusu kuanzisha bustani na kutunza miche ya miti kwa wadau mbalimbali 17 kutoka Dar es Salaam, Gairo, Manispaa ya Morogoro, Turiani, Mafinga, Manispaa ya Iringa na Korogwe.

**(ix) Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)**

**80. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imefanya utafiti juu ya ubora wa mbao za miti ya mitiki na misindano iliyovunwa katika umri tofauti kwenye Mashamba ya Miti Longuza, Mtibwa, Kiwira na Kawetire. Utafiti umeonesha kuwa, miti aina ya mitiki kutoka Shamba la Longuza inaweza kuvunwa kati ya miaka 30 hadi 32 badala ya miaka 40 ya awali kutegemea hali ya rutuba na mvua. Katika umri unaopendekezwa, utafiti umeonesha kuwa ubora na ujazo wa mbao hauna tofauti na miti yenye umri zaidi, hivyo kuacha miti shambani kwa zaidi ya miaka 32 ni kuongeza gharama za uzalishaji. Aidha, utafiti wa miti ya misindano katika Mashamba ya Kiwira na Kawetire umeonesha kuwa inaweza kuvunwa kati ya miaka 18 kwa Kiwira na miaka 20 kwa Kawetire kutoka miaka 25 hadi 30 ya awali. Kwa matokeo haya, wakulima wa miti kwa maeneo yenye hali ya hewa inayoshabihiana na maeneo yaliyofanyiwa utafiti wanashauriwa kuzingatia umri wa uvunaji miti uliopendekezwa.

**81. Mheshimiwa Spika,** Taasisi imeendelea kutoa elimu kuhusu uanzishaji wa bustani za miti na mashamba kwa ajili ya kuni na mkaa. Elimu hiyo imetolewa katika vijiji vinne vya Mvuleni na Mwarusembe (Mkuranga) na Kwamatuku na Muungano B (Handeni) ambapo wakulima 120 wamenufaika. Kutokana na elimu hiyo, kila kijiji kimeanzisha shamba darasa lenye eneo la hekta moja. Aidha, wananchi 120 kwenye vijiji hivyo wameanzisha bustani za miti na wanazihudumia wenyewe.

**82. Mheshimiwa Spika,** mwaka 2014/2015, Taasisi iliendelea kuboresha mazingira, miundombinu na vitendea kazi. Kazi zilizofanyika ni uwekaji wa samani za ofisi na ukumbi wa mikutano; ufungaji wa mawasiliano ya TEHAMA ya kitafiti na mawasiliano ya kawaida; na ununuzi wa kompyuta. Aidha, Taasisi imewawezesha watumishi 10 kuhudhuria mafunzo ya muda mrefu. Kati ya

watumishi hao, mmoja ni Astashahada, wawili Shahada na saba Shahada ya Uzamivu.

### **iii. Sekta Ndogo ya Utalii**

#### **a. Sera na Sheria**

**83. Mheshimiwa Spika,** Wizara imezifanyia marekebisho Kanuni za Kuendesha Biashara za Utalii nchini kwa kuzingatia maoni ya wadau yaliyopatikana kwenye warsha iliyofanyika Oktoba, 2014. Aidha, mapitio ya Sera ya Taifa ya Utalii ya mwaka 1999 yanaendelea na mikutano mitatu ya mashauriano na wadau imefanyika. Mpango wa utekelezaji wa kazi hiyo na hadidu za rejea za kumpata Mtaalamu Mwelekezi atakayeandaa rasimu ya sera hiyo umeandaliwa.

#### **b. Mwenendo wa Sekta**

**84. Mheshimiwa Spika,** mwaka 2014, idadi ya watalii walioingia nchini ilikuwa 1,140,156 ikilinganishwa na 1,095,884 mwaka 2013. Watalii hao walitembelea vivutio mbalimbali hapa nchini na kuliingizia Taifa Dola za Kimarekani bilioni 1.9 ikilinganishwa na 1.8 zilizopatikana mwaka 2013. Kutokana na zoezi la kuhakiki huduma za malazi kwa watalii nchini lililofanyika katika mikoa 16, imebainika kuwa kuna vitanda 33,330. Mikoa yenye idadi kubwa ya vitanda ni Dar es Salaam (10,231), Arusha (5,188), Tanga (2,762), Kilimanjaro (2,704), Manyara (2,604) na Dodoma (2,193).

#### **c. Usimamizi wa Biashara za Utalii**

**85. Mheshimiwa Spika,** Wizara iliendesha zoezi la ukaguzi wa Wakala wa biashara za utalii katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Mara, Arusha, Iringa na Manyara. Zoezi hilo liliwezesha uboreshaji wa kanzi ya huduma za malazi na Dola za Kimarekani 12,000 zilikusanywa kutoka kwa Wakala waliobainika kuendesha biashara kinyume cha sheria.

#### **d. Bodi ya Utalii (TTB)**

**86. Mheshimiwa Spika,** mwezi Oktoba 2014, Bodi ya Utalii iliandaa onesho jipya la kimataifa liitwalo Swahili International Tourism Expo (S!TE) lililofanyika Dar es Salaam. Onesho hilo lilikuwa na washiriki kutoka nchi 13 za Afrika, Asia, Ulaya, Amerika na Australia. Waoneshaji 40 na wawakilishi 21 wa wakala wa huduma za utalii wa kimataifa na wageni kutoka nchi mbalimbali duniani

wakiwemo wanahabari, wanadiplomasia na watoa huduma za usafiri walishiriki.

**87. Mheshimiwa Spika,** Bodi ilishiriki maonesho ya kimataifa ya utalii, ikiwemo onesho la ITB (Ujerumani), INDABA (Africa Kusini), WTM (Uingereza) na COTTM (China). Katika maonesho hayo, Bodi ilishirikiana na wadau kutoka Taasisi za Umma na Sekta Binafsi katika kutangaza vivutio vya Tanzania. Bodi ilifanya misafara nchini Marekani, Uswizi, na China ili kuhamasisha watalii kuja kutembelea vivutio vya utalii nchini. Hatua hii ni utekelezaji wa Mkakati wa Utangazaji Utalii 2012 – 2016 ambao umeainisha nchi ambazo Tanzania inatakiwa kujitangaza zaidi.

**88. Mheshimiwa Spika,** Bodi kwa kushirikiana na TANAPA imeendelea kuhamasisha upandaji wa Mlima Kilimanjaro ili kuutangaza vizuri zaidi. Desemba 2014, kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bodi iliandaa safari ya kupanda Mlima kwa Mabalazi 19 wanaowakilisha Tanzania nje ya nchi. Wakati wa maadhimisho ya miaka 50 ya ushirikiano baina ya Tanzania na China (Februari 2015), Bodi iliratibu safari ya kupanda Mlima kwa washiriki 51 (wachina 45 na watanzania 6) ambayo iliwahusisha waandishi wa habari na wawakilishi kutoka Kampuni za Utalii.

**89. Mheshimiwa Spika,** katika kutangaza utalii nje ya nchi kupitia sekta ya michezo, Bodi iliingia mkataba na klabu ya mpira wa miguu ya Sunderland ya Uingereza. Matangazo yameoneshwa katika uwanja wa timu hiyo kuanzia Agosti 2014 hadi Mei, 2015. Wizara imekamilisha Andiko la kunadi utalii (branding) na tangazo la televisheni litaanza kurushwa kupitia vituo vya CNN na “BBC World” kuanzia Juni, 2015. Wizara kupitia Bodi ya Utalii imeanzisha “portal” kwa ajili ya kutangaza utalii na “Apps” itakayowezesha kupatikana taarifa za utalii Tanzania kupitia simu za viganjani. Aidha, Bodi iliendelea kuwawezesha mabalazi watatu wa heshima (Tourism Goodwill Ambassadors) katika nchi ya Marekani (2) na Australia (1) kutangaza utalii wa Tanzania kwenye nchi zao.

**90. Mheshimiwa Spika,** ushauri wa kitaalamu katika utalii wa utamaduni ulitolewa kwa vikundi na jamii mbalimbali. Elimu na ushauri huo, umetolewa katika maeneo 16 ya Simangoni, Minjingu, Kamwaha, Babati, Hanang, Longido, Materuni, Rau, Mto wa Mbu, Haydom four covers, Machame, Soweto-Moshi, Tengeru, Mulala, Engaresero na Kondoa Irangi. Ili kuhamasisha watanzania kushiriki

katika utalii wa utamaduni na kukuza Sekta ya Utalii, Bodi kwa kushirikiana na Channel Ten kupitia kipindi cha “Mimi na Tanzania” ilitangaza utalii wa kiutamaduni wa maeneo ya Tengeru, Mulala na Mto wa Mbu.

**e. Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT)**

**91. Mheshimiwa Spika,** Wakala umedahili jumla ya wakurufunzi 218. Kati ya hao, wakurufunzi 68 wapo Kampasi ya Bustani, 91 Kampasi ya Temeke na 59 Kampasi ya Arusha. Aidha, Wakala ulifanya mafunzo ya kozi ya awali kwa wakurufunzi 11 ambao walijiunga na Chuo katika ngazi ya Stashahada.

**iv. Sekta Ndogo ya Malikale**

**a. Uhifadhi na Uendelezaji wa Rasilimali za Kale**

**92. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuboresha mazingira ya vituo vya Mambo ya Kale vya Isimila na Kalenga Mkoani Iringa na Kwihara Mkoani Tabora. Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa mitaro ya maji kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko wa udongo na ukarabati wa makumbusho ndogo katika Kituo cha Isimila. Jengo la zamani, Kalenga limekarabatiwa na sasa linatumika kama ofisi ya Kituo cha Makumbusho ya Chifu Mkwawa - Kalenga. Katika Kituo cha Kwihara kazi ya ukarabati wa Tembe ilifanyika. Aidha, Wizara imesaini mkataba na mtaalamu Mshauri ili kuandaa michoro kwa ajili ukarabati wa majengo ya Pangani na kujenga Kituo cha Taarifa na Kumbukumbu Amboni.

**93. Mheshimiwa Spika,** ninayo furaha kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, baada ya kufanyiwa ukarabati, eneo la magofu ya Kilwa Kisiwani na Songo Mnara limerejeshewa hadhi yake ya kuwa katika Orodha ya UNESCO ya Urithi wa Dunia. Maamuzi hayo yalifikiwa katika Mkutano wa 38 wa Kamati ya Urithi wa Dunia chini ya UNESCO uliofanyika tarehe 15 hadi 25 Juni, 2014 nchini Qatar. Aidha, Ukumbi wa Nkurumah wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam umeingizwa katika Orodha ya Urithi wa Dunia.

**b. Ushiriki katika Mikutano ya Kikanda na Kimataifa**

**94. Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni mwanachama wa mashirika ya uhifadhi wa Malikale ya “International Council on Monuments and Sites (ICOMOS)” na “International Center for the Study of Preservation and Restoration of Cultural Property (ICCROM)”.

Kutokana na uanachama huo, katika mwaka 2014/2015, Wizara ilishiriki katika Mikutano Mikuu ya Taasisi hizo iliyofanyika Novemba, 2014 (ICOMOS), Florence, Italia na Novemba 2014 (ICCROM) Roma, Italia. Wizara ilishiriki Mkutano wa Kanda ya Afrika kuhusu Uhifadhi wa Urithi wa Utamaduni uliomo majini, uliofanyika Malindi, Kenya Machi, 2015.

**c. Mfuko wa Taifa wa Mambo ya Kale**

**95. Mheshimiwa Spika,** Mfuko ulikadiria kukusanya **Sh.1,100,000,000** kutoka vyanzo vyake kwa 2014/2015. Hadi Machi 2015, Mfuko umekusanya **Sh.826,613,644** sawa na asilimia 75 ya makadirio. Fedha za Mfuko zilielekezwa katika ukarabati wa vituo, utafiti na utangazaji wa vivutio vya Mambo ya Kale katika maonesho nje na ndani ya nchi.

**d. Shirika la Makumbusho ya Taifa Tanzania (NMT)**

**96. Mheshimiwa Spika,** katika kuitangaza na kuisogeza makumbusho karibu na jamii, Shirika liliandaa na kufanya programu shirikishi 11 kuhusu urithi wa utamaduni na historia ya Taifa. Programu hizo zilihusisha matamasha, midahalo, warsha na semina. Vilevile, Shirika liliandaa maonesho 11, ikijumuisha onesho la kumuenzi Hayati Rashid Mfaume Kawawa, “Simba wa Vita: Kawawa Mzalendo Aliyetukuka” lililofanyika sambamba na maadhimisho ya kumbukumbu ya vita ya Maji Maji Februari, 2015. Aidha, liliandaa mdahalo kuhusu mchango wa Hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius K. Nyerere juu ya kujenga, kulinda na kutetea amani ambao ulifanyika katika kuadhimisha kumbukumbu ya kifo cha Baba wa Taifa Oktoba, 2014.

**97. Mheshimiwa Spika,** Shirika limeendelea kutoa vitendea kazi na motisha kwa watumishi ili waweze kutekeleza kazi zao kwa ufanisi. Shirika limewezesha watumishi watatu kuhudhuria mafunzo katika Shahada ya Uzamili na Stashahada. Vilevile, watumishi waliwezesha kushiriki mafunzo ya muda mfupi kuhusu “curation of art”, kuhifadhi nyaraka za makumbusho kielektroniki (digitization of archives) na huduma kwa mteja. Watumishi wawili walihudhuria mafunzo ya muda mfupi ya uhifadhi pamoja na mafunzo ya maonesho nchini China.

**98. Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Upanuzi wa Makumbusho na ushirikishaji wa wadau umeendelea kutekelezwa kupitia uanzishaji wa Makumbusho ya Baba wa Taifa, Mwalimu J.K. Nyerere ya Falsafa ya Ujamaa na Kujitegemea huko Chamwino, Dodoma. Shirika

limepata eneo la ekari 22 Kititimo, Manispaa ya Singida ili kuanzisha Makumbusho ya Kanda yenye bustani ya wanyama na kituo cha michezo ya watoto. Aidha, familia ya Hayati Rashid Mfaume Kawawa imetoa nyumba ya Bomba Mbili Songea ili iwe Makumbusho.

**v. Uratibu, Utawala na Maendeleo ya Rasilimaliwatu**

**99. Mheshimiwa Spika,** mwaka 2014/2015, Wizara imeendelea kusimamia masuala ya watumishi ikiwemo utendaji kazi na nidhamu. Ili kukabiliana na upungufu wa watumishi hasa wa kada ya Wahifadhi Wanyamapori, Wizara ilipewa kibali cha kuajiri watumishi 1,077 wa kada mbalimbali. Kutokana na kibali hicho watumishi 466 walijiriwa, kati ya hao 453 ni wa kada ya Wahifadhi Wanyamapori. Nafasi zilizobaki zitajazwa kabla ya mwaka wa fedha kumalizika.

**100. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza ufanisi na kuboresha utendaji, Wizara imewezesha watumishi 177 kuhudhuria mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Kati ya hao watumishi 97 wamehudhuria mafunzo ya muda mrefu na 80 mafunzo ya muda mfupi. Aidha, watumishi 182 wa kada mbalimbali wamepandishwa cheo; watumishi 73 wamethibitishwa kazini; na watumishi 6 wamebadilishiwa Muundo wa Utumishi.

**101. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kuimarisha Chama cha Kuweka na Kukopa ambapo watumishi waliojiunga tayari wameanza kuchangia kupitia makato ya mishahara. Watumishi waliojitokeza wanaoishi na virusi vya UKIMWI wameendelea kupatiwa fedha kwa ajili ya kununua virutubisho na lishe bora ili kuimarisha afya zao. Kwa lengo la kuboresha afya za watumishi na kujenga mahusiano mazuri na watumishi wengine wa umma, Wizara imewezesha watumishi 48 kushiriki michezo ya SHIMIWI iliyofanyika mkoani Morogoro Septemba hadi Oktoba, 2014; Watumishi 22 kushiriki Siku ya Wanawake Duniani Machi, 2015; na watumishi 38 kushiriki michezo ya Mei Mosi iliyofanyika Mwanza.

**vi. Ukusanyaji Maduhuli**

**102. Mheshimiwa Spika,** mwaka 2014/15 Wizara ilikadiri kukusanya jumla ya **Sh.158,790,010,023** kupitia Idara, Mifuko na Taasisi zilizo chini yake. Hadi Machi 2015, Wizara ilikusanya jumla ya **Sh.112,004,867,786** sawa na asilimia 71 ya lengo.

**IV. CHANGAMOTO ZA SEKTA NA MIKAKATI YA KUZIKABILI**

**103. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu ya Wizara Changamoto mbalimbali zilijitokeza. Changamoto hizo ni pamoja na ujangili na biashara haramu ya nyara; migogoro ya mipaka na uvamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa na matumizi yasiyo endelevu ya rasilimali za maliasili na malikale. Changamoto nyingine ni uvunaji haramu wa mazao ya misitu na ukwepaji ulipaji tozo za utalii; ubovu wa miundombinu kama barabara, nyumba za watumishi, viwanja vya ndege na madaraja katika maeneo yaliyohifadhiwa; uhaba wa watumishi na vitendea kazi; mwamko mdogo wa Watanzania kutembelea vivutio vya Utalii. Kutokana na tishio la ugaidi katika ukanda wa Afrika Mashariki pamoja na mlipuko wa ugonjwa wa Ebola, baadhi ya wageni waliahirisha safari za utalii.

**104. Mheshimiwa Spika,** Wizara imejipanga kushirikisha wadau mbalimbali katika uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili, malikale na shughuli za utalii. Ili kutatua migogoro ya mipaka na uvamizi katika maeneo yaliyohifadhiwa, Wizara itaendelea kurekebisha na kuweka alama za kudumu katika mipaka, kufanya doria katika maeneo yaliyohifadhiwa na kutoa elimu ya uhifadhi kwa Umma pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani. Aidha, Wizara itaendelea kuboresha mifumo ya ukusanyaji na ufuatiliaji wa maduhuli. Vilevile, Wizara itaendelea na jitihada za kuongeza idadi ya watumishi, kutoa mafunzo na kuongeza vitendea kazi. Katika kutangaza utalii, kampeni za Kimataifa zitatumika kuwatoa hofu wageni kuhusu usalama wao nchini.

## **V. MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2015/2016**

**105. Mheshimiwa Spika,** mapendekezo ya mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 yamezingatia maelekezo yanayolenga kutekeleza sera na mikakati ya Serikali. Malengo na kazi za Wizara yamejikita katika maeneo sita ya kipaumbele yaliyoainishwa katika Mpango Mkakati wa Wizara (2013-2016). Kwa muhtasari, Wizara imejipanga kutekeleza yafuatayo:

### **i. Sekta Ndogo ya Wanyamapori**

**106. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaanzisha Maabara ya “GIS and Remote Sensing” kwa lengo la kuratibu shughuli za doria. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kubaini fursa mpya za uwekezaji na kuandaa mkakati wa kuzitangaza; kutafuta maeneo kwa ajili ya ujenzi wa Makao Makuu ya TAWA na Ofisi za Kanda. Aidha, Kanuni za Usajili wa Nyara na Kanuni za Usimamizi wa Shoroba, Kingo na

Mapito ya Wanyamapori kwa ajili ya kutekeleza sheria ya wanyamapori zitakamilishwa.

**107. Mheshimiwa Spika,** Wananchi wanaoishi katika maeneo yanayopakana na hifadhi za wanyamapori wataendelea kuhamasishwa kushiriki katika uanzishaji na usimamizi wa maeneo ya Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori (WMAs). Kufuatia ufumbuzi wa Migogoro ya mipaka, Wizara itafanya tathmini ya mali za wananchi ili kulipa fidia kwa wananchi waliohamishwa kutoka Pori la Akiba Mkungunero. Aidha, doria zitafanyika nje na ndani ya Mapori 28 ya Akiba; maeneo 10 ya Mapori Tengefu pamoja na maeneo yanayosumbuliwa na wanyamapori wakali na waharibifu.

#### **a. Vyuvo vya Taaluma ya Wanyamapori**

**108. Mheshimiwa Spika,** vyuvo vya mafunzo ya uhifadhi wanyamapori vitadahili jumla ya wakurufunzi 1,220, ambapo Chuo cha Usimamizi na Uendelezaji wa Wanyamapori Mweka kitadahili wakurufunzi 720 na Chuo cha Taaluma ya Wanyamapori Pasiansi wakurufunzi 500. Katika kuimarisha miundombinu na vitendea kazi, Chuo cha Mweka kitanunua magari mawili kwa ajili ya kuhudumia safari za mafunzo kwa vitendo. Aidha, Chuo cha Pasiansi kitaendelea na ujenzi wa jiko na mabweni. Kituo cha Elimu ya uhifadhi wanyamapori kwa jamii Likuyu Sekamaganga kitatoa mafunzo kwa wananchi 250.

#### **b. Taasisi ya Utafiti Wanyamapori Tanzania (TAWIRI)**

**109. Mheshimiwa Spika,** mwaka 2015/2016 Taasisi itaendeleza utafiti wa mbwa mwitu katika mfumo-ikolojia wa Serengeti na kuendelea kuhamasisha jamii kulinda na kuhifadhi wanyama hawa wasitoweke. Tafiti za mwenendo wa magonjwa ya wanyamapori, na magonjwa ya maambukizo baina ya binadamu, wanyamapori na mifugo zitaendelezwa. Aidha, utengenezaji wa mizinga 1,300 iliyoboreshwa kiutafiti itasambazwa kwa wadau wa sekta ya ufugaji nyuki nchini.

#### **c. Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA)**

**110. Mheshimiwa Spika,** Shirika kwa kushirikiana na Bodi ya Utalii Tanzania litaendelea kutangaza vivutio vipya vilivyoibuliwa ikiwemo maeneo maalum katika Hifadhi ya Serengeti. Aidha, mfumo wa wageni kulipa ada kwa njia ya ki-elektroniki wakati wa kuingia kwenye hifadhi utaendelea kuboreshwa na kutumika kwenye hifadhi zote.



**111. Mheshimiwa Spika,** Shirika litajenga nyumba 40 za watumishi katika hifadhi mbalimbali nchini. Vilevile, Shirika litaboresha barabara ndani ya hifadhi zenye urefu wa kilometa 4,500 na viwanja vya ndege saba. Katika kuboresha ulinzi na uhifadhi, Dawati Maalum la Intelijensia na Kikosi Maalum cha Mbwa wa kunusa na kufuatilia mienendo ya majangili ndani ya maeneo ya hifadhi litaimarishwa. Aidha, Shirika litafunga mfumo wa kisasa wa mawasiliano. Vilevile, Shirika litanunua silaha na vifaa vya kisasa ili kuimarisha ulinzi wa wanyamapori na kutekeleza Mpango wa 'Moru Defence Plan' katika Hifadhi ya Taifa Serengeti. Shirika litajenga mabanda ya watalii yenye uwezo wa vitanda 230 kwa ajili ya wageni hususan utalii wa ndani. Mabanda hayo yatajengwa katika Hifadhi za Taifa Tarangire, Serengeti, Saadani, Ruaha, Mikumi, Kilimanjaro na Rubondo.

#### **d. Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA)**

**112. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka itaendelea na shughuli za uhifadhi wa wanyamapori na malikale, kuhudumia jamii ya wafugaji na kuendeleza shughuli za utalii. Mamlaka itanunua magari matano kwa ajili ya doria na huduma za utalii; itakarabati nyumba mbili za askari; na kujenga ofisi na choo katika uwanja wa ndege Nduu. Vilevile, kilometa 407 za barabara zilizoko ndani ya eneo la hifadhi zitatengenezwa na kukarabatiwa.

**113.** Mamlaka itaendelea kutekeleza mradi wa kuhifadhi nyayo za Zamadamu za Laetoli; mradi wa kuboresha mifugo; kukamilisha mradi wa Kijiji cha Jema walikohamishiwa wahamiaji waliotolewa katika hifadhi na kuukabidhi kwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro. Aidha, Mamlaka itanunua magunia 30,700 ya mahindi kwa ajili ya jamii zinazoishi katika Hifadhi. Ujenzi wa jengo la Kitega Uchumi jijini Arusha utaendelezwa.

#### **ii. Sekta Ndogo ya Misitu na Nyuki**

**114. Mheshimiwa Spika,** Wizara itakamilisha mapitio ya Sera ya Ufugaji Nyuki kwa mwaka 2015/2016. Aidha, itafanya uchambuzi wa Sheria ya Misitu na ya Ufugaji Nyuki mara baada ya mchakato wa mapitio ya Sera kukamilika. Wizara itaandaa Programu mpya ya misitu na nyuki ya 2016-2021.

#### **a. Vyuo vya Taaluma ya Misitu na Ufugaji Nyuki**

**115. Mheshimiwa Spika,** Vyuho vya Misitu na Ufugaji Nyuki vinatarajia kudahili jumla ya wakurufunzi 426 kama ifuatavyo: Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki Tabora 100; Chuo cha Misitu Olmotonyi – Arusha 266 na Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi 60. Wakufunzi wawili wa Chuo cha Ufugaji Nyuki Tabora watawezesha kuhudhuria mafunzo ngazi ya shahada ya uzamili. Pia, Chuo cha Viwanda vya Misitu kitaongeza vifaa vya kisasa vya karakana na kuwajengea uwezo watumishi watatu.

**116. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha miundombinu, Chuo cha Mafunzo ya Ufugaji Nyuki kitajenga nyumba moja ya mtumishi na kukarabati madarasa mawili, mabweni matatu na maktaba. Vilevile, kitachimba kisima cha maji pamoja na kutengeneza mfumo wa uvunaji maji ya mvua. Aidha, Chuo kitaanzisha manzuki mbili kwa ajili ya mafunzo. Chuo cha Viwanda vya Misitu Moshi kitajenga maktaba na kukarabati mabweni mawili, madarasa mawili na bwalo la chakula. Chuo cha Misitu Olmotonyi kitakarabati ukumbi wa mikutano, bwalo la chakula, nyumba sita za watumishi, jengo moja la kuchakata magogo na jengo moja la kutengeneza samani.

#### **b. Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania (TAFORI)**

**117. Mheshimiwa Spika,** Taasisi itaendelea kutafiti na kushauri kuhusu umri sahihi ambao mti unastahili kuvunwa na ubora wa mbao kutoka katika mashamba ya miti ya misindano ya Rongai, Meru, West Kilimanjaro, Rubya na Buhindi. Aidha, taasisi itaandaa mbinu bora za Kilimo-Misitu kwa kuwashirikisha wakulima wanaolima kwenye miteremko ya milima ya Uluguru. Baadaye mbinu hizo kuenezwa katika sehemu nyingine za miteremko.

**118. Mheshimiwa Spika,** Taasisi itaendeleza kuimarisha uwezo wa vituo vyake kwa kuanza ujenzi wa ofisi za vituo vya Tabora na Dodoma. Vilevile, itaweka mfumo wa maji ya bomba katika majengo ya Taasisi, Makao Makuu na kununua magari manne. Katika kuongeza ufanisi wa kazi, watumishi 10 watawezesha kuhudhuria mafunzo ya muda mfupi na mrefu. Aidha, Taasisi itaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali katika kuendeleza mpango wa uboreshaji wa mazao ya misitu kwa kutumia miche ya miti iliyoboreshwa.

#### **c. Wakala wa Mbegu za Miti Tanzania (TTSA)**

**119. Mheshimiwa Spika,** Wakala utakusanya kilo 12,500 za mbegu za miti na kuuza kilo 11,500 za mbegu pamoja na miche 100,000. Mbegu zitakazouzwa ni pamoja na Msindano, Mkangazi, Mtiki, Mwerezi, Mkenge, Mgunga na Mkongo. Aidha, miche itakayouzwa ni pamoja na Mitiki, Miembe, Michungwa, Mikangazi na Mwalambe. Wakala utaanzisha vyanzo vitano vya mbegu bora za miti na kutambua na kusajili vyanzo vitatu vya mbegu za miti ya Mkenge na Mgunga. Wakala utaendelea kutunza vyanzo 35 vya mbegu za miti ya aina mbalimbali. Wakala utaendesha mafunzo ya muda mfupi kuhusu kuanzisha bustani na kutunza miche ya miti kwa wadau.

**d. Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)**

**120. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaandaa mipango ya uvunaji kwenye eneo la hekta 100,000; utawezesha Kamati za Uvunaji za Wilaya 46 kufanya mikutano ya kupitisha maombi ya wavunaji; na kudhibiti uvunaji haramu wa mazao ya misitu. Vilevile, utafanya tathmini ya rasilimali za misitu; kuandaa mipango ya usimamizi ya misitu 18; na kufanya mapitio ya mipango minne ya misitu katika Kanda za Nyanda za Juu Kusini, Mashariki, Kusini, Kati na Kaskazini.

**121. Mheshimiwa Spika,** ili kusimamia na kuongoa maeneo yaliyovamiwa, Wakala utaondoa wavamizi katika misitu ya hifadhi 33; kufanya mapitio ya soroveya na kusafisha mipaka ya misitu ya hifadhi 70 yenye urefu wa kilomita 4,116; kuweka maboya 690 na mabango 459 ili kutoa tahadhari kwa jamii kuhusu maeneo yaliyohifadhiwa. Kazi nyingine ni kupanda miti kwenye eneo la hekta 484 za misitu ya asili na hekta 162 za eneo la mikoko; na kuotesha miti kwenye mipaka yenye urefu wa kilomita 200 za misitu. Vilevile, Wakala utafanya tathmini ya rasilimali za misitu katika Msitu wa Hifadhi Mangalisa, Dodoma na kurejea kupima kongano (clusters) 200 katika Kanda za Magharibi na Nyanda za juu Kusini. Aidha, Wakala utahakiki, kuhuisha na kuweka mfumo wa kidijitali kwa ramani za misitu ya asili 41 na hifadhi za misitu asilia 11.

**122. Mheshimiwa Spika,** Katika jitihada za kuongeza mapato, Wakala utaendelea kuboresha vivutio vya utalii ikolojia kwa kutunza miundombinu katika hifadhi asilia. Uboreshaji huo utahusisha kutengeneza barabara za kwenye misitu zenye urefu wa kilomita 60; njia za kuvinjari zenye urefu wa kilomita 176; vituo vinne vya kuangalia mandhari; na kambi 21 za kupumzikia wageni katika hifadhi asilia tano na misitu ya asili miwili. Vilevile, Wakala utapandisha hadhi Msitu wa Hifadhi Mlima Hanang kuwa Hifadhi ya Mazingira Asilia.

**123. Mheshimiwa Spika,** Wakala utaotesha miche ya miti 17,994,360, kutayarisha hekta 8,041 na kupanda hekta 11,774 katika maeneo mapya, maeneo yaliyovunwa na maeneo yaliyokufa miti. Kazi nyingine zitakazofanyika ni kupalilia hekta 33,037, kupogoa hekta 8,258 na kupunguza miti hekta 2,171. Barabara zenye urefu wa kilomita 1,845 zitakarabatiwa na kilomita 67 zitajengwa katika mashamba ya miti. Nyumba 86 na mifumo ya maji katika mashamba 13 zitafanyiwa ukarabati. Vilevile, hekta 5,000 zitaongezwa katika eneo la Makongotema na Wino.

**124. Mheshimiwa Spika,** ulinzi wa mashamba ya miti utafanyika kwa kufanya doria, kusafisha mipaka ya urefu wa kilomita 4,421 ili kuzuia moto na kuweka maboya 340 kwenye mipaka. Aidha, minara mitatu kwa ajili ya kubaini matukio ya moto itajengwa na 51 iliyopo kuendelea kutunzwa. Vilevile, kampeni 78 zitafanyika kuhamasisha jamii inayozunguka mashamba ya miti juu ya madhara na kinga dhidi ya moto.

**125. Mheshimiwa Spika,** Elimu kwa umma itatolewa kupitia maonesho ya Sabasaba, Nanenane, Siku ya Kupanda Miti na Utundikaji Mizinga Kitaifa. Wakala pia utaandaa vipindi 82 vya redio na 32 vya televisheni. Katika juhudi za kulinda uoto wa asili kampeni za kuzuia moto zitafanyika kwa viongozi wa vijiji 112 vilivyo kando ya misitu ya hifadhi 20. Elimu ya usimamizi na matumizi ya rasilimali za misitu itatolewa kwa kamati 89 za maliasili za vijiji na pia kuwezesha kuanzishwa kwa kamati 18.

**126. Mheshimiwa Spika,** katika kuongeza msukumo wa upandaji miti kwa jamii, Wakala utaandaa programu ya uhifadhi wa mazingira na kuwezesha vikundi 177 kuotesha na kupanda miche 8,400,000. Wakala pia utafanya mapitio na kuandaa mipango 23 ya makubaliano ya usimamizi wa pamoja wa misitu na mipango 41 ya usimamizi wa misitu ya vijiji.

**127. Mheshimiwa Spika,** Wakala utasimamia na kuendeleza manzuki 88 zenye mizinga 6,214; kuanzisha manzuki nne na kutundika mizinga 540. Katika kudhibiti ubora wa mazao ya nyuki elimu itatolewa kwa wafugaji nyuki 610, vikundi 400 vya ufugaji nyuki, wachakataji na wafanyabiashara wa mazao ya nyuki katika kanda saba za Wakala. Sampuli 70 za asali zitakusanywa na kufanyiwa uchambuzi wa kimaabara. Vilevile, Wakala utawezesha usajili na kuanza kazi kwa Chama cha Kuendeleza Ufugaji Nyuki Tanzania.

**e. Mfuko wa Misitu Tanzania (TaFF)**

**128. Mheshimiwa Spika,** Mfuko unakadiria kukusanya **Sh.6,486,171,000** kutoka vyanzo vyake vya mapato. Mfuko utatoa ruzuku kwa miradi 217 ya wadau wa misitu na ufugaji nyuki ikiwemo miradi mipya 139. Aidha, Mfuko utaendelea kugharimia ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi iliyopewa ruzuku.

**iii. Sekta Ndogo ya Utalii**

**129. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kuendesha biashara ya utalii pamoja na kuongeza ukusanyaji mapato. Katika kuboresha mazingira hayo, Kanuni za Kuendesha biashara ya Utalii zitakamilishwa. Vilevile, Wizara itafanya ukaguzi kwa wakala wa biashara za utalii katika kanda nne ili kutambua wanaofanya biashara hiyo kinyume na taratibu zilizowekwa na hatua zinazostahili kuchukuliwa dhidi yao.

**130. Mheshimiwa Spika,** ili kuwezesha jamii kunufaika na biashara ya utalii, Wizara itafanya tathmini ya uendeshaji wa biashara za utalii kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati katika mikoa ya Pwani, Kilimanjaro na Arusha. Aidha, Wizara itafanya utafiti wa hali ya utalii nchini ili kupata picha kamili ya mwenendo wa sekta ya utalii.

**a. Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)**

**131. Mheshimiwa Spika,** Bodi itaongeza jitihada za utangazaji katika nchi zinazoinukia kiuchumi kama vile China, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), India na Brazil. Vilevile, Bodi itaendelea kusimamia na kuendeleza onesho la kimataifa la Utalii la Swahili International Tourism EXPO (SITE). Jitihada za kuhamasisha mashirika ya ndege kuja Tanzania zitaendelezwa na Bodi kwa kushirikiana na Mamlaka ya viwanja vya ndege Tanzania (TAA) na wadau wengine. Aidha, Bodi inatarajia kuongeza idadi ya mabalozi wa hiari kutoka watatu hadi saba. Mabalozi hao watatoka katika nchi za Italia, Uingereza, Ujerumani na China.

**b. Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT)**

**132. Mheshimiwa Spika,** kutokana na tofauti ya mafunzo yanayotolewa na vyuo vingi vya utalii vinavyochipukia nchini, ilionekana kuwa kuna haja ya kufanya utafiti na kubaini suluhisho la changamoto hiyo. Wakala umepata Mtaalam mwelekezi kwa ajili ya kufanya tathmini ya mahitaji ya mafunzo kwa wakufunzi wa vyuo

vyote vinavyotoa mafunzo ya ukarimu na utalii nchini. Kazi hiyo imeanza Mei, 2015 na itakapokamilika Wakala utaandaa mafunzo kwa wakufunzi wa vyuo.

**133. Mheshimiwa Spika,** Wakala unatarajia kutoa mafunzo kwa Wakurufunzi 312 wa ngazi ya Stashahada na Astashahada na kuandaa mitaala ya mafunzo kwa programu za Shahada za Utalii na Ukarimu. Taratibu za kupata utambulisho wa Kimataifa (ISO *certification*) kwa ajili ya kuthibitisha ubora na kuwezesha kukubalika kwa Chuo kimataifa zinafanyika.

#### **iv. Sekta Ndogo ya Malikale**

**134. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaandaa miongozo ya uhifadhi wa miji ya kihistoria ya Kilwa Kivinje, Mikindani na Pangani; na kuendelea kuboresha kanzi ya kitaifa kuhusu urithi wa maeneo ya wapigania uhuru katika Mkoa wa Mtwara. Kazi nyingine ni kufanya ukarabati wa Boma la Pangani; kuanza ujenzi wa Kituo cha Taarifa na Kumbukumbu cha Amboni; kutengeneza mandhari ya Makumbusho ya Kumbukizi ya Dkt. Livingstone - Ujiji na ujenzi wa uzio katika Kituo cha Kunduchi-Dar es Salaam.

#### **a. Shirika la Makumbusho ya Taifa (NMT)**

**135. Mheshimiwa Spika,** Shirika litaendelea kuboresha Maonesho na kuhakikisha usalama wa mikusanyo na mali za Shirika, kufanya Tamasha la Utamaduni la Mtanzania kwa kushirikisha jamii ya Wanyasa, kuitangaza Makumbusho na kusogeza huduma kwa jamii. Shirika litatoa elimu na ushauri wa kitaalamu kwa jamii, kufanya utafiti na kuhifadhi mikusanyo. Ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa watumishi hususani wataalamu wa kazi za Kimakumbusho, Shirika linatarajia kuajiri watumishi 21.

#### **v. Uratibu, Utawala na Maendeleo ya Rasilimaliwatu**

**136. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatarajia kuajiri jumla ya watumishi 1,091. Kati ya hao, 965 ni wa kada ya Wahifadhi Wanyamapori na Misitu. Aidha, watumishi 420 watathibitishwa na kupandishwa cheo kwa kuzingatia miundo ya Utumishi. Wizara itaendelea kutoa mafunzo kwa kuzingatia mpango wa mafunzo.

**137. Mheshimiwa Spika,** katika kuboresha ustawi na afya za watumishi, Wizara itaendelea kuwawezesha watumishi wanaoishi na

virusi vya UKIMWI kupata huduma ya lishe. Wizara itaendelea kushirikiana na wadau kutoa elimu na kuhamasisha watumishi kupima kwa hiari VVU na magonjwa sugu yasiyoambukizwa ili kutambua hali za afya zao na kuchukua hatua stahiki.

**138. Mheshimiwa Spika,** Wizara itaendelea kuwashirikisha watumishi katika vikao na maonesho mbalimbali na kuandaa mikutano miwili ya Baraza la Wafanyakazi. Watumishi watawezesha kushiriki katika mashindano ya michezo SHIMIWI na Mei Mosi.

**139. Mheshimiwa Spika,** Wizara inatarajia kufanya mapitio ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara (2013-2016) na kuandaa Mpango Mkakati (2016-2021). Wizara itaratibu na kusimamia mfumo wa kielektroniki utakaowezesha kuunganisha taarifa za maduhuli kupatikana katika kituo kimoja. Katika kutoa elimu kwa umma, Wizara itaendelea kuchapisha jarida na vipeperushi mbalimbali vya kuelezea Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Maliasili, Malikale na Utalii.

## **VI. SHUKRANI**

**140. Mheshimiwa Spika,** kabla ya hitimisho la hotuba yangu, napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa wananchi hususan wanaoishi kwenye maeneo yanayopakana na hifadhi. Ushiriki wao katika kulinda rasilimali za maliasili na malikale umechangia uwepo wa rasilimali hizo kwa maendeleo ya nchi. Nachukua nafasi hii kuwaomba kuendelea kushirikiana nasi katika kuendeleza sekta hii.

**141. Mheshimiwa Spika,** majukumu yote niliyoyaeleza yametekelezwa kwa ushirikiano mzuri baina ya viongozi na watumishi wote wa Wizara. Shukurani za pekee nazielekeza kwa Mhe. Mahmoud Hassan Mgimwa-Naibu Waziri, Mbunge wa Mufindi Kaskazini; Dkt. Adelhelm James Meru-Katibu Mkuu na Bw. Selestine Gesimba-Naibu Katibu Mkuu kwa ushirikiano wanaoutoa kwangu. Nawashukuru kwa dhati watumishi wote wa Wizara na wadau wa sekta kwa juhudi wanazoonsha katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara.

**142. Mheshimiwa Spika,** Wizara imetekeleza majukumu yake kwa ushirikiano na wadau wa maendeleo kutoka nchi na asasi mbalimbali za kitaifa na kimataifa na sekta binafsi. Nichukue fursa hii kuwashukuru wote na kutaja baadhi ya wadau kama ifuatavyo: Marekani, Ujerumani, Uingereza, Sweden, Ufaransa, Ubelgiji, Japan, Norway, Finland, Jumuiya ya nchi za Ulaya, DANIDA, UNDP/GEF, FAO, UNWTO, ILO, World Bank, KfW, GIZ, IUCN, UNESCO, ICCROM,

JICA, ICOMOS, ICOM, WMF, BTC, HBF, WWF, FINNIDA, FZS, AWF, AWHF, SNV, AFD, USAID, Trade Aid na NORAD.

## **VII. HITIMISHO**

**143. Mheshimiwa Spika**, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya jumla ya **Sh. 81,964,541,000** kwa mwaka 2015/2016. Kati ya fedha hizo, **Sh. 74,255,391,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Sh. 7,709,150,000** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Fedha za Matumizi ya Kawaida zinajumuisha **Sh.45,235,955,000** za Mishahara ya watumishi na **Sh.29,019,436,000** za Matumizi Mengineyo. Fedha za Miradi ya Maendeleo zinajumuisha **Sh.5,709,150,000** fedha za nje na **Sh.2,000,000,000** fedha za ndani.

**144. Mheshimiwa Spika**, Naomba kutoa Hoja.



**Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka 2015/2016**

<b>Kifungu</b>	<b>Idara/Kitengo/Taasisi</b>	<b>Mishahara (Sh.)</b>	<b>Matumizi Mengineyo (Sh.)</b>	<b>Jumla (Sh.)</b>
1001	Utawala na Rasilimaliwatu	2,680,932,000	2,518,510,000	5,199,442,000
1002	Fedha na Uhasibu	890,039,000	988,000,000	1,878,039,000
1003	Sera na Mipango	295,032,000	948,500,000	1,243,532,000
1004	Mawasiliano	32,820,000	358,224,000	391,044,000
1005	Ukaguzi wa Ndani	168,061,000	406,592,000	574,653,000
1006	Ugavi	231,026,000	348,358,000	579,384,000
1007	Sheria	173,316,000	255,784,000	429,100,000
1008	Mifumo ya Kompyuta	61,282,000	435,042,000	496,324,000
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>4,532,508,000</b>	<b>6,259,010,000</b>	<b>10,791,518,000</b>
<b>2001</b>	<b>Wanyamapori</b>	11,672,333,000	5,965,016,000	17,637,349,000
270321	Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori -TAWIRI	2,182,860,000	790,400,000	2,973,260,000
270323	Chuo cha Wanyamapori - Mweka	2,053,889,000	711,400,000	2,765,289,000
270368	Chuo cha Wanyamapori - Likuyu Sekamaganga	-	237,200,000	237,200,000
270369	Chuo cha Wanyamapori - Pasiansi	-	276,700,000	276,700,000
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>15,909,082,000</b>	<b>7,980,716,000</b>	<b>23,889,798,000</b>
<b>3001</b>	<b>Misitu na Nyuki</b>	1,024,701,000	663,934,000	1,688,635,000
270370	Taasisi ya Utafiti wa Misitu -TAFORI	2,124,479,000	1,817,913,000	3,942,392,000
270610	Wakala wa Mbegu wa Taifa -TTSA	377,796,000	474,300,000	852,096,000
270373	Chuo cha Taifa cha Ufugaji Nyuki - BTI	-	474,300,000	474,300,000
270371	Chuo cha Misitu Olmotonyi - FTI	-	513,800,000	513,800,000
270372	Chuo cha Viwanda vya Misitu - FITI	-	687,700,000	687,700,000
270631	Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS)	14,049,192,000	-	14,049,192,000
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>17,576,168,000</b>	<b>4,631,947,000</b>	<b>22,208,115,000</b>
<b>4001</b>	<b>Utalii</b>	674,052,000	2,213,111,000	2,887,163,000
270501	Bodi ya Utalii Tanzania (TTB)	2,037,506,000	3,475,739,000	5,513,245,000
270321	Wakala wa Chuo cha Taifa cha Utalii (NCT)	1,755,274,000	1,817,913,000	3,573,187,000
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>4,466,832,000</b>	<b>7,506,763,000</b>	<b>11,973,595,000</b>
<b>4002</b>	<b>Mambo ya Kale</b>	853,678,000	1,107,000,000	1,960,678,000
270834	Shirika la Makumbusho ya Taifa (NMT)	1,897,687,000	1,534,000,000	3,431,687,000
	<b>Jumla Ndogo</b>	<b>2,751,365,000</b>	<b>2,641,000,000</b>	<b>5,392,365,000</b>
	<b>JUMLA KUU</b>	<b>45,235,955,000</b>	<b>29,019,436,000</b>	<b>74,255,391,000</b>

**Jedwali Na. 2: Mauzo ya Asali na Nta Nje ya Nchi Mwaka 2009/2010 - 2013/2014**

Mwaka	Nta		Asali	
	Tani	Thamani (US\$)	Tani	Thamani (US\$)
2009/2010	329.9	1,427,680	291.4	457,639
2010/2011	534.0	2,598,826	343.0	646,250
2011/2012	418.4	2,473,461	208.5	644,253
2012/2013	241.3	1,520,560	93.1	406,518
2013/2014	422.4	3,201,631	126.7	211,694

**Jedwali Na. 3: Hali ya Mashamba ya Miti Yanayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania kwa Mwaka 2015**

Na.	Jina la Shamba	Mahali	Eneo lililopandwa (Ha)	Eneo la upanuzi (Ha)	Eneo lenye Misitu ya Asili	Ujazo (kwa tathmini ya 2012/13 - m <sup>3</sup> )
1	Buhindi	Sengerema	4,322	7,057	10,880	261,095
2	Kawetire	Mbeya	2,372	276	1163	137,439
3	Kiwira	Rungwe	2,784	45	-	334,290
4	Korogwe	Handeni	100	10,705	-	-
5	Longuza	Muheza	1,904	200	409	242,450
6	Mbizi	Sumbawanga	696	10,904	-	-
7	Meru	Arumeru	6,110	-	1629	548,954
8	Mtibwa	Mvomero	2,025	-	746	149,274
9	North Kilimanjaro	Rombo	6,177	200	504.7	563,941
10	Rondo	Lindi	864	1,541	-	13,869
11	Rubare	Bukoba	1,727	1,420	11,742.30	23,275
12	Rubya	Ukerewe	1,771	181	2924	243,930
13	Ruvu kaskazini	Kibaha	53	31,947	-	-
14	Sao Hill	Mufindi	53,975	34,098	49,900	8,341,371
15	Shume	Lushoto	4,227	140	84.1	510,792
16	Ukaguru	Kilosa	976	941	-	60,189
17	West Kilimanjaro	Hai	4,149	337	3294.8	377,601
18	Wino	Songea	2,080	9,300	-	129.89
	<b>Jumla</b>		<b>96,313</b>	<b>109,292</b>	<b>83,277</b>	<b>11,808,600.89</b>

**Jedwali Na. 4: Mwenendo wa Biashara ya Utalii nchini 2010-2014**

<b>MWAKA</b>	<b>2010</b>	<b>2011</b>	<b>2012</b>	<b>2013</b>	<b>2014</b>
Idadi ya watalii	782,699	867,994	1,077,058	1,095,884	1,140,156
Idadi ya watalii hotelini	719,097	753,818	974,448	1,021,766	1,054,338
Mapato ( US \$ million)	1,254.50	1,324.83	1,712.75	1,853.28	1,982.98
Wastani wa siku za kuka watalii hotelini	11	10	10	10	10
Wastani wa matumizi ya fedha kwa mtalii kwa siku(US \$)	328 <sup>1</sup>	355 <sup>1</sup>	384 <sup>1</sup>	372 <sup>1</sup>	378 <sup>1**</sup>
	236 <sup>2</sup>	247 <sup>2</sup>	230 <sup>2</sup>	201 <sup>2</sup>	210 <sup>2**</sup>

<sup>1</sup> Package Tour

<sup>2</sup> Non Package Tour

\*\* Provisional figure

**Jedwali Na. 5: Idadi ya Watalii Waliotembelea Hifadhi za Taifa kuanzia Mwaka 2010/2011 hadi 2014/2015**

<b>Mwaka wa Fedha</b>	<b>Idadi ya Watalii wa Nje</b>	<b>Idadi ya Watalii wa Ndani</b>	<b>Jumla ya Watalii</b>
2010/2011	540,440	333,294	873,734
2011/2012	586,869	360,928	947,797
2012/2013	537,675	364,217	901,892
2013/2014	530,142	427,207	957,350
2014/2015*	425,741	325,658	751,399

\*takwimu za hadi Machi, 2015

**Jedwali Na. 6: Idadi ya Watalii Waliotembelea Hifadhi ya Ngorongoro Mwaka 2010/2011 hadi 2014/2015**

<b>Mwaka</b>	<b>Idadi ya Watalii wa Ndani</b>	<b>Idadi ya Watalii wa Nje</b>	<b>Jumla</b>
2010/2011	271,577	281,407	552,984
2011/2012	260,953	333,577	594,530
2012/2013	285,888	344,964	630,852
2013/2014	275,121	341,755	619,876
2014/2015*	219,064	261,185	480,249
<b>Jumla</b>	<b>1,956,741</b>	<b>2,854,695</b>	<b>5,033,217</b>

\* takwimu za hadi Machi, 2015

**Jedwali Na. 7: Idadi ya Vyumba na Vitanda kwa Mikoa 16 kwa Mwaka 2014/2015**

<b>Na.</b>	<b>Mkoa</b>	<b>Idadi ya Vyumba</b>	<b>Idadi ya Vitanda</b>
1	Arusha	3,394	5,188
2	Dar es Salaam	8,758	10,231
3	Kilimanjaro	1,719	2,704
4	Tanga	1,005	2,762
5	Mwanza	1,394	1,555
6	Mara	144	169
7	Morogoro	1,107	1,183
8	Pwani	617	495
9	Lindi	161	219
10	Mtwara	493	544
11	Iringa	591	805
12	Mbeya	1,152	1,270
13	Manyara	1,357	2,604
14	Tabora	581	585
15	Singida	788	823
16	Dodoma	2146	2193
<b>Jumla</b>		<b>25,407</b>	<b>33,330</b>

*\*takwimu hizi ni kwa zoezi lililofanyika Septemba, 2014 hadi Aprili, 2015*

**Jedwali Na. 8: Idadi ya Watalii Waliotembelea Vituo vya Mambo ya Kale na Mapato kwa Mwaka 2011/2012 - 2013/2014**

<b>Kituo</b>	<b>2011/2012</b>		<b>2012/2013</b>		<b>2013/2014</b>	
	<b>Wageni</b>	<b>Mapato (Sh.)</b>	<b>Wageni</b>	<b>Mapato (Sh.)</b>	<b>Wageni</b>	<b>Mapato (Sh.)</b>
Olduvai George	59,515	320,179,614	38,343	1,016,434,514	42,557	995,615,000
Kaole	23,745	17,480,000	25,138	26,691,000	46,102	40,000,000
Isimila	3,767	3,744,000	3,124	5,420,500	4,443	9,513,500
Mji Mkongwe	8,575	5,593,100	24,390	16,551,500	14,484	13,913,000
Kalenga	4,355	4,044,000	3,618	3,696,000	2,170	5,261,000
Kilwa	1,963	1,653,700	2,052	15,288,850	2,112	15,610,900
Mbozi	1,582	1,498,200	990	811,000	893	1,361,000
Amboni	11,717	7,432,300	13,488	14,844,500	27,073	26,015,000
Tongoni	628	718,000	1,659	4,176,000	397	898,200
Ujiji	3,283	11,959,500	3,319	5,770,700	4,937	9,411,300
Kwihara	1,083	957,000	542	468,000	428	495,000
Kolo	1,071	870,800	514	1,327,000	1,239	6,844,500
Caravan Serai	6,873	4,633,300	6,670	7,019,000	8,095	7,499,000
<b>Jumla</b>	<b>124,260</b>	<b>379,348,714</b>	<b>123,847</b>	<b>1,124,048,564</b>	<b>154,930</b>	<b>1,132,327,400</b>

**Jedwali Na. 9: Idadi ya Watalii Waliotembelea Vituo vya Makumbusho na Mapato kuanzia Mwaka 2013 Hadi 2014**

Kituo	Wageni 2013			Mapato (Sh.)	Wageni 2014			Mapato (Sh.)
	Nje	Ndani	Jumla		Nje	Ndani	Jumla	
Makumbusho na Nyumba ya Utamaduni	7,033	82,931	89,964	207,157,835	8,593	121,752	122,611	147,516,927
Kijiji cha Makumbusho	3,516	10,103	13,619	61,604,411	3,339	11,061	14,397	81,805,911
Makumbusho ya Azimio la Arusha	107	37,037	37,144	18,104,551	343	14,033	14,377	8,967,120
Makumbusho ya Elimu Viumbe	3,149	13,759	16,908	39,481,300	1,639	6,905	9144	42,801,446
Makumbusho ya Mwalimu Nyerere	234	6,686	6,920	4,722,350	125	7980	8,105	292,684
Makumbusho ya Vita ya Majimaji	65	2,478	2,543	1,402,000	61	3,994	4,055	2,188,548
<b>JUMLA</b>	<b>14,104</b>	<b>152,994</b>	<b>167,098</b>	<b>332,472,447</b>	<b>14,127</b>	<b>165,725</b>	<b>199,683</b>	<b>283,572,638</b>

**Jedwali Na. 10: Idadi ya Wakurufunzi Waliodahiliwa katika Vyuo vya Wizara 2010/2011 - 2014/2015**

Chuo Mwaka	Misitu na Nyuki			Utalii	Wanyamapori			Jumla
	FITI - Moshi	BTI - Tabora	FTI - Olmotonyi	NCT	Mweka	Pasiansi	Likuyu Sekamaganga	
2010/2011	21	34	147	237	453	224	178	1,294
2011/2012	23	39	166	229	502	284	200	1,443
2012/2013	31	57	145	249	502	324	70	1,378
2013/2014	32	40	167	242	540	400	189	1,610
2014/2015	30	79	266	218	616	415	83	1,114
<b>JUMLA</b>	<b>158</b>	<b>249</b>	<b>1,029</b>	<b>1,175</b>	<b>2,939</b>	<b>1,759</b>	<b>1,116</b>	<b>7,982</b>

**Jedwali Na. 11: Makisio ya Fedha Zinazopelekwa Hazina na Zinazobakizwa katika Mifuko na Taasisi kwa Mwaka 2015/2016**

Idara	Makisio 2015/2016			Jumla (Sh.)
	Hazina (Sh.)	Mifuko (Sh.)	Taasisi (Sh.)	
Utawala na Rasilimali Watu	31,001,000	-	-	31,001,000
Wanyamapori	17,102,340,614	25,432,794,020 <sup>1</sup>	8,443,194,535	50,978,329,169
Idara ya Misitu na Nyuki (Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania)	30,500,001,000	6,486,171,000	52,374,682,982	89,360,854,982
Utalii	15,907,000,000	-	1,903,181,000	17,810,181,000
Mambo ya Kale	1,000,000,000	-	500,442,575	1,500,442,575

<sup>1</sup> Inajumuisha TWPF na Pori la Akiba Selous

Idara	Makisio 2015/2016			Jumla (Sh.)
	Hazina (Sh.)	Mifuko (Sh.)	Taasisi (Sh.)	
<b>JUMLA KUU</b>	<b>64,540,342,614</b>	<b>31,918,965,020</b>	<b>63,221,501,092</b>	<b>159,680,808,726</b>

**Jedwali Na. 12: Mwenendo wa Ukusanyaji Maduhuli katika Sekta Ndogo ya Wanyamapori kwa Mwaka 2010 hadi 2014**

Maelezo		2010	2011	2012	2013	2014
Uwindaji wa Kitalii	USD	14,443,417	13,375,780	10,768,056	16,255,674	9,146,335.44
Utalii wa Picha	USD	2,576,677	7,975,452	2,854,370	4,566,708	3,811,423
	Sh.	128,704,850	408,873,272	32,075,365	27,533,000	280,443,900
Leseni ya Biashara za Nyara	Sh.	16,122,000	20,707,000	17,719,914	52,000,000	7,762,900
Vibali vya kusafirishia Nyara Nje ya Nchi	Sh.	14,705,750	14,529,768	9,752,456	34,133,596	1,440,750
Vibali vya Kukamata Wanyamapori	Sh.	137,055,190	65,665,766	5,372,060	200,760,325	200,558,929
Hati za Kumiliki Nyara	Sh.	2,231,840	1,752,330	3,012,887	9,038,661	1,005,250
Ada Nyinginezo	Sh.	15,174,066	7,228,219	8,939,516	17,879,032	13,271,694
<b>Jumla</b>	USD	<b>17,020,094</b>	<b>21,351,232</b>	<b>13,622,426</b>	<b>20,822,382</b>	<b>12,957,758</b>
	Sh.	<b>313,993,696</b>	<b>518,756,355</b>	<b>76,872,198</b>	<b>341,344,614</b>	<b>504,483,423</b>